epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Ijumaa Novemba 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581875

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUMU

# Mabingwa Zanzibar, Muhimbili wafichua sumu za kope bandia



• **Madhara** yake; saratani, upofu, macho mekundu... *Endelea ukurasa 4*



Amiri Jeshi Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na viongozi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kabla ya kuwatunuku maofisa wanafunzi Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (BMS) kundi la 05/21 katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (TMA) Monduli, mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Samia atunuku kamisheni kwa maofisa 236 JWTZ, wamo wanawake 40

UKURASA 2

UKURASA WA 2

**Nduguliile** kuzikwa Kigamboni Jumanne ijayo, wengi wamlilia



UKURASA WA 7

**SGR** yaingiza bilioni 28.5/- miezi mitano



UKURASA WA 7

**Shahidi** huru kesi dawa za kulevya abanwa kizimbani 'kulikoni kila siku shuhuda ni yeye?'

## Vigogo wa CHADEMA waitana kwa dharura kutafakari Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAPANIA KUREJEA KWA KASI LIGI KUU UK.24 **MAONI,** UK.6

# Wengi wamlilia Dk. Ndugulile, mwili kuwasili leo

**Na Restuta James**



WATU mbalimbali wakiwamo wabunge wa Dar es Salaam na wakazi, wamemlilia aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile, wakieleza kuwa alikuwa mtu mwenye upendo na mwenye kupenda ushirikiano.

Dk. Ndugulile aliyezaliwa Machi 31, 1969, alifariki dunia juzi akiwa nchini India alikokwenda kutibiwa na mwili wake unatarajiwa kuwasili leo mchana. Mwili wa Dk. Ndugulile, ambaye alikuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, utazikwa katika makaburi ya Mwongozo, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Msemaji wa familia ambaye ni mdogo wake, Wilbert Ndugulile, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba mwili wa Dk. Ndugulile, utawasili nchini leo saa 6:35 mchana.

Aidha, kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Ofisi ya Bunge jana, mwili huo utapokewa na Naibu Spika, Mussa Azan Zungu, Katibu wa Bunge, wajumbe wa Tume ya Bunge, wawakilishi wa serikali na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ratiba hiyo inaonesha kwamba mwili utapelekwa moja kwa moja Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo na kuhifadhiwa hadi Jumapili utakapopelekwa nyumbani kwake, Kigamboni.

Nyumbani kwa marehemu ambako ni takribani mita 200 kutoka kivuko cha Kigamboni, jana vilitawala huzuni na majonzi, huku wananchi na viongozi wa CCM, wabunge na watumishi wa manispaa ya Kigamboni, wakijumuika kuifariji familia.

Baadhi ya wananchi waliozungumza nyumbani kwa marehemu, walisema Dk. Ndugulile alikuwa mtu wa watu, akiwapigania wananchi wake na kutoa ushauri bila hila.

Walisema mbunge huyo alisimamia kile alichokiamini bila kuvunja sheria wala wakubwa zake.

Mbunge wa Mbagala (CCM), Abdallah Chaurembo, alisema Dk. Ndugulile alikuwa kiongozi aliyependa kushirikiana na alisikiliza ushauri wa watu wengine.

Alisema Dk. Ndugulile alikuwa mtu wa matokeo na alipenda kuona maendeleo yakifanyika na kuonekana.

Wabunge wengine waliofika nyumbani kwa marehemu ni mbunge wa Kinondoni, Tarimba Abass, viongozi wa CCM mkoa na wilaya za Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Meya wa Manispaa ya Kigamboni, Ernest Mafimbo, alisema kwa mujibu wa ratiba ya Bunge, wananchi wa jimbo la Kigamboni wataaga mwili wa Dk. Ndugulile katika viwanja vya Machava keshokutwa.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, Jumatatu ataongoza waombolezaji kuaga mwili wa Dk. Ndugulile katika viwanja vya Karimjee kwenye heshima za kiserikali ambazo zitahudhuriwa na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa likiwamo la Afya Duniani (WHO), wabunge na mawaziri.

Wilbert ambaye ni msemaji wa familia kuhusu msiba huo, alisema jana kwamba baada ya mwili kuwasili na kupelekwa Lugalo, familia, ndugu jamaa na rafiki, wataendelea na maombolezo nyumbani kwake, Kigamboni.

"Baada ya mwili kuwasili na kupelekwa Lugalo, familia tutaendelea na maombolezo hadi tarehe 2 Desemba. Mwili utatolewa Lugalo na kupelekwa Parokia ya Mtakatifu Imaculata Upanga kwa ajili ya ibada. Baada ya hapo mwili utapelekwa Karimjee kwenye mazishi ya kitaifa," alisema.

Alisema baada ya Karimjee, mwili utalala nyumbani kwake Kigamboni na Jumenne, mwili utapelekwa viwanja vya Machava kwa ajili ya wananchi kumuaga.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Watoto walio chini ya Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, wakijifunza kutengeneza keki na mkate wa nazi juzi, katika mafunzo yanayotolewa na kituo hicho mara mbili kwa mwezi yakiambatana na ufundishaji wa mambo mbalimbali ikiwamo namna ya kugundua viashiria vya ukatili, utunzaji mazingira na stadi za maisha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia atunuku kamisheni maofisa 236 JWTZ, wamo wanawake 40

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Dk. .Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, jana aliwawatunuku kamisheni kwa maofisa wanafunzi 236 wa cheo cha Luteni Usu, kutoka kundi la 5/2021 la Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (BMS) na kundi la 71/23 (Regular) katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA).

Kabla ya kutunuku kamisheni hizo, Rais Samia alikagua gwaride lililoandaliwa na maofisa wanafunzi hao ambao kati yao wanaume ni 196 na wanawake 40.

Katika maofisa hao waliotunukiwa cheo cha Luteni Usu kutoka kundi la 5/2021 BMS ambao jumla yao ni 75 na wamepata mafunzo chuoni hapo kwa miaka mitatu na kuhitimu shahada ya sayansi ya kijeshi.

Vilevile, katika kundi la 71/23 - Regular, maofisa wapya 95 wamepata mafunzo yao kwa muda wa mwaka mmoja na maofisa 88 wamepata mafunzo ya kijeshi kutoka nchi rafiki za Afrika na nje ya bara la Afrika.

Pia alitunuku shahada ya kwanza ya sayansi ya kijeshi kwa maofisa wapya 75 ambao kati yao wanaume 53 na wanawake 22.

Baada ya kutunuku kamisheni hizo, Rais alitoa zawadi kwa maofisa waliofanya vizuri katika fani mbalimbali. Katika kundi la 05/21 BMS, aliyefanya vizuri katika fani zote kwa ujumla ni Luteni Usu Cloud Ndaiga.

Kadhalika, aliyefanya vizuri katika taaluma ni Luteni Usu Xavery Malobana na aliyefanya vizuri katika Medani ni Luteni Usu Kelvin Adrian, huku aliyefanya vizuri kutoka nchi rafiki ni Luteni Usu Thabi Masuku kutoka Eswatini.

Kwa kundi la 71/23-Regular, aliyefanya vizuri katika fani zote ni Luteni Usu John Bahati na katika taaluma Luteni Usu Charles Charles. Katika medani, aliyefanya vizuri ni Luteni Usu Apha Gustav.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk.Stergomana Tax, alisema mafunzo ya shahada ya sayansi ya kijeshi ni muhimu kwa jeshi lakini pia kwa taifa.

"Umuhimu wa mafunzo haya unajidhihirisha kwenye umahiri wa jeshi letu katika kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Mafunzo haya huwajengea uwezo wa kutekeleza operesheni za kijeshi kwa ustadi mkubwa na kuwaandaa kuwa viongozi wenye maadili, nidhamu na weledi wa kuongoza vikosi vya jeshi," alisema.

Waziri Tax alisema kitaifa mafunzo hayo huhakikisha jeshi linapata viongozi wazalendo na wenye uwezo wa kulinda mipaka ya nchi na kukabiliana na vitisho vya ndani na nje ya nchi.

"Kwa ujumla, mafunzo haya yanajenga jeshi imara na taifa lenye uwezo wa kudumisha amani, usalama na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi," alisema.

Mkuu wa TMA, Meja Jenerali Jackson Mwaseba, aliwakumbusha wahitimu kutambua kuwa jeshi na taifa limewekeza fedha na rasilimali nyingi kwao ili kuhakikisha wanapata elimu bora kwa ajili ya manufaa yao binafsi, jeshi na taifa kwa ujumla.

"Taifa linahitaji wasomi walio na uzalendo, nidhamu, maadili mema ambao wataingia kujenga nchi yetu kwa misingi endelevu, hivyo wahitimu mna dhamana kubwa ya kutumia taaluma zenu katika kutimiza wajibu wenu kutekeleza kwa vitendo," alisema Jenerali Mwaseba.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




# Wakulima, wafugaji wapewa angalizo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis amewataka wakulima na wafugaji nchini kufanya shughuli zao bila kuharibu mazingira.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dodoma wakati akiongoza kikao na Ujumbe wa Tanzania ambao utashiriki katika Mkutano wa 16 wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame unaotarajiwa kufanyika jijini Riyadh, Saudi Arabia.

Khamis alisema vitendo vya baadhi ya wakulima kukata miti ovyo na kuchoma misitu kwa ajili ya kuandaa na kusafisha mashamba na wafugaji kulisha mifugo kiholela, huchangia ukame na hatimaye kuwapo tishio la maeneo mengi kuwa jangwa.

Naibu Waziri aliwataka wakulima na wafugaji nchini kuacha kuhamahama kwa kuwa kitendo hicho kinachochea hatari ya kuenea kwa jangwa.

"Wakulima na wafugaji wanapokata miti na kulisha mifugo, wanapohamahama wanaacha maeneo yakiwa yameharibiwa, hivyo ninawaomba waache kufanya hivyo, wanasababisha maeneo mengi kukabiliwa na hali ya ukame na jangwa," alisisitiza.

Khamis alisema pamoja na kuwa ufugaji na kilimo ni sekta kubwa zinazokuza uchumi na kutangaza nchi, wafugaji na wakulima wanao wajibu wa kuhakikisha wanafuata sheria za mazingira na hivyo kupunguza ongezeko la jangwa.

Aliwaomba wafugaji waache kuchunga au kunywesha mifugo kwenye vyanzo vya maji kwa kuwa kwa kufanya hivyo, wanasababisha uharibifu wa mazingira, maji kukauka na kuleta ukame.

Naibu Waziri huyo pia aliwasisitiza wafugaji na wananchi kwa ujumla kupanda miti na kuitunza ili kusaidia kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba nchi na dunia.

Alisema hali ni mbaya kwa sababu maeneo mengi wananchi wamekata miti ovyo na kuchangia ukosefu wa mvua na hivyo ukame kukithiri katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Hivyo, Naibu Waziri Khamis alisema kuwa kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa mazingira, serikali itaendelea na jitihada za kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuacha shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Hassan Mitawi, alisema mkutano huo wa kupambana na hali ya jangwa ni muhimu kwa Tanzania.

Alisema Tanzania kupitia wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, wizara za kisekta na wadau wa maendeleo itakuwa katika nafasi nzuri ya kushiriki kikamilifu kwa mustakabali wa nchi.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Agnes Meena na wataalamu mbalimbali kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, wizara za kisekta na Mkurugenzi wa Taasisi ya LEAD Foundation, Njamasi Chiwanga.




Naibu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), anayesimamia Taaluma Utafiti na Ushauri Kitaalamu, Prof. Richard Kangalawe (kushoto), akizungumza katika Kusanyiko la Baraza la Wahitimu (Convocation), waliosoma katika chuo hicho, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Kusanyiko hilo, Gelard Mwamsiku na Mhadhiri kutoka Idara ya Lugha na Fasihi ya chuo hicho, Dk. Ahmad Sovu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vigogo CHADEMA wajifungia kutafakari Uchaguzi S/Mitaa

## -Mwenyekiti wa CCM adaiwa kuchomwa kisu

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeitisha kikao cha dharura cha Kamati Kuu ya Chama kujadili kilichojiri katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika juzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, kauli ya chama kuhusu uchaguzi huo itatolewa baada ya kikao hicho.

"Kamati Kuu ya Chama itakutana kwa kikao cha dharura kesho (leo). Kikao hicho kitajadili ajenda maalumu ya yaliyojiri kwenye kinachoitwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji 2024 na hatimaye kutoka na msimamo wa chama. Kauli ya chama itatolewa baada ya kikao hicho kumalizika," alisema Mrema.

Alisema kikao hicho kitaongozwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freema Mbowe.

Kikao hicho kimeitishwa wakati CHADEMA ikiwa miongoni mwa vyama vilivyoshiriki uchaguzi huo, ikiwa na malalamiko ya kuwapo kasoro kwenye uchaguzi huo.

Miongoni mwa madai ya chama hicho ni wagombea na mawakala wao kukamatwa vituoni na katika maeneo mengine kuchelewa kuanza kupiga kura kwa madai ya kuchelewa kufikishwa kwa karatasi za kura au kuchanganya vitabu vyenye orodha ya wapiga kura, vingine kupelekwa kituo A au B.

Madai mengine ya chama hicho ni kukamatwa karatasi ambazo tayari zilibainika kuwa zina kura zilizopigwa kabla ya kuanza kwa zoezi la upigaji kura.

Wakati huo, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, amezitaka mamlaka kuwaachia bila masharti viongozi na makada wa chama hicho wanaoshikiliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**ACHOMWA KISU**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Ikana, wilayani Momba, Amos Sikamanga (41), amelazwa katika Kituo cha Afya Tunduma, akidaiwa kujeruhiwa kwa kuchomwa kisu cha utosi na wanaodaiwa viongozi wa CHADEMA.

Tukio hilo lilitokea juzi saa tatu asubuhi katika eneo la kituo cha kupigia kura cha Nakawale, kijijini Nakawale.

Akizungumza kwa njia ya simu, Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Wilaya ya Momba, Chuki Sichalwe, alidai mwenyekiti wao huyo alijeruhiwa kwa kuchomwa na kisu kichwani sehemu ya utosi alipofika katika kituo hicho cha kupigia kura cha Nakawale kwa lengo la kukagua mawakala wa chama hicho wakati zoezi la kupiga kura linaendelea.

"Viongozi hao wa CHADEMA walikuwa wanamzuia mwenyekiti wetu kuingia katika chumba cha mawakala wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ofisi hizo, hivyo kuzuka vurugu zilizosababisha kuchomwa kisu," alidai Sichalwe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Augostino Senga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba tayari jeshi hilo linawashikilia viongozi wawili wa CHADEMA kwa tuhuma za kuhusika na tukio hilo.

Kamanda Senga aliwataja viongozi hao wa CHADEMA wanaoshikiliwa ni Gidion Siame (34) ambaye ni Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Momba na Fiston Haonga (57) ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee (BAZECHA) Jimbo la Momba, wote wakazi wa kijiji cha Nakawale, wilayani humo.

Akifafanua zaidi kuhusu tukio hilo, Kamanda Senga alisema uchunguzi wa awali unaonesha chanzo cha tukio hilo ni mihemuko ya kisiasa.

Alidai kuwa watuhumiwa walikuwa wanamzuia mwathirika kuingia katika chumba cha mawakala wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ofisi ya kijiji cha Nakawale.

"Mwathirika yuko Kituo cha Afya Tunduma anaendelea na matibabu na uchunguzi wa tukio hili unaendelea na pindi utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani," alisema Kamanda Senga.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Moses Ng'wat (SONGWE).**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Mabingwa wa Zanzibar, Muhimbili waorodhesha madhara kope bandia

## -Zimo saratani, upofu, macho mekundu...
## -Utafiti: Kila harusi kope bandia zatawala
## -Serikali yaanza rasmi kutoa elimu mitaani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UBANDIKAJI kope bandia umeshika kasi visiwani Zanzibar. Lakini wataalamu wanaonya kuwa zinaweza kusababisha saratani ya macho, upofu, uoni hafifu na jicho kuvimba.

Kwa utafiti wa Nipashe kisiwani Unguja uliojikita maeneo yenye sherehe za harusi mwezi uliopita, kati ya wanawake 10, watano walibandika kope bandia wakati wa sherehe.

Salim Hamad Kassim, Mkuu wa Divisheni ya Vipodozi katika Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) amemwambia mwandishi wa habari hizi kwamba, wamebaini kuwapo idadi kubwa ya wanawake wanaobandika kope bandia visiwani humu, wengi wao ni wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 45.

Ofisa huyo wa ZFDA ana angalizo kwa kundi hilo kwamba, kope asilia kwa binadamu zina kazi ya kulinda macho dhidi ya mwanga, vumbi na vitu vingine; kope bandia hutumika kama urembo lakini wengi wanatumia urembo huo pasi na kujua madhara yake.

Anasema kinacholeta madhara zaidi katika ubandikaji kope ni gundi ambayo lazima itumike wakati wa ubandikaji kope bandia.

"Gundi hiyo hutengenezwa kwa kemikali tofauti kama vile Cyanoacrylate, Rubeber Latex, Acrylate Copolymer, Latex Free Polymer na Formaldehyde Free Formulate. Zote hizi zina athari kwa binadamu na zina vichocheo vya saratani," Kassim anaonya.

Ofisa huyo wa ZFDA anasema kuna aina nne za gundi ambazo hutumika kubandika kope, akizitaja kwa lugha ya taaluma yake: "Clear eyelash glue, Blac eyelash glue, Non latex eyelash glue na waterproof eyelash glue".

Kassim anaendelea kufafanua, akisema: "Miongoni mwa athari ambayo mtumiaji anaweza kupata ni kuwa na uzio katika jicho, uvimbe katika jicho, maambukizi ya macho, maambukizi ya bakteria na fangasi, hali ambayo inaweza kupelekea saratani ya jicho.

Anasema aina hizo na gundi hutumika kwa matumizi tofauti lakini isivyo bahati wananchi huchukulia gundi zote matumizi yake ni sawa, hata kuweka hatarini kwa afya zao.

"Zipo gundi ambazo zinaweza kutumika ambazo hazina madhara makubwa na zimethibitishwa kuwa hazina kemikali zenye sumu, mfano gundi ya waterproof eyelash glue," alisema.

Kutokana na wimbi kubwa la watumiaji gundi katika kupandika kope bandia, Kassim anasema ZFDA inatarajia kutoa elimu kwa jamii. Maofisa wao watakuwa wanapita shuleni na sehemu nyingine yenye mikusanyiko ya



watu ili kuwapa elimu kuhusu matumizi ya gundi na athari zake.

"Tumezoea kutoa elimu ya vitu vikubwa, tukasahau vitu vidogo lakini kiuhalisia si vidogo katika afya na wengi wao wanachukulia gundi ni kitu cha kawaida.

"Hivi sasa kunashuhudiwa kasi ya ongezeko la wanawake wanaobandika kope bandia. Kuna ongezeko kubwa, hasa ikizingatiwa kuwa sherehe ni nyingi na watu wanataka kuonekana wamependeza. Kwa hiyo, tunataka tuwafikishia ujumbe kabla gundi hiyo haijaleta madhara makubwa," anasema.

Kassim anasema ufuatiliaji wa ZFDA umebaini wabandikaji kope bandia visiwani Zanzibar kwa asilimia 100 ni wanawake, hivyo hata mpango wao wa kutoa elimu juu ya madhara ya urembo huo itakijita kwa kundi hilo.

Anasema watengenezaji wa gundi hiyo ni kampuni za China na Marekani, lakini zinapoingizwa nchini lazima zifuate utaratibu na gundi zilizopo zinatambulika kuwa zimeingizwa kihalali na wakaguzi huchukua sampuli kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi ili kulinda afya ya mtumiaji.

Anasema kemikali ya "formaidehde" ambayo hutumika katika gundi ni kichocheo cha saratani na gundi yenye kemikali hiyo huzuiwa isitumike, lakini "baadhi ya wafanyabiashara huingiza nchini kwa udangayifu".

Kassim anasema tayari ZFDA imepokea kesi nne za watu waliopata madhara baada ya kutumia gundi yenye kemikali ya "Latex", wakipata mwasho katika jicho, lakini baadaye walitibiwa wakapona na kushauriwa kuacha kutumia gundi kubandikia kope.

Nini kifanyike? Ofisa huyo wa ZFDA anawataka waingizaji wa vipodozi kufuata taratibu zilizowekwa na lazima bidhaa hizo zifanyiwe uchunguzi. Watumiaji nao wafuate maelekezo ya matumizi ya gundi.

"Watumiaji wahakikishe wazitambua kemikali zilizomo katika gundi husika na kuwa makini na matumizi yake, wafuate maelekezo ya kutumia gundi. Wale walioathirika baada ya kutumia gundi hizo, wafike ZFDA," alielekeza.

**UTANDAWAZI**

Rajab Muhammed Hilali, Mratibu wa Huduma za Afya ya Macho Msingi kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, anasema utandawazi umesababisha wimbi kubwa la wanawake kubandika kope na wengine hubandika hadi kiini cha jicho cha bandia, hali anayoitaja ni hatari kwa afya zao.

Anasema hupokea wastani wa watu wanne kwa mwezi ambao hufuata matibabu ya macho kutokana na ubandikaji kope bandia, wengi wao wakipata michubuko katika jicho.

Hilali anawataka wanawake wenye tabia ya kubandika kope kuchukua tahadhari kwa kuwa kope bandia zinaweza kuwaletea madhara.

Anasema madhara hugundulika mapema zaidi kwa wanaobandika kisha kulala na kope bandia au kiini cha jicho cha bandia.

"Maendeleo yanakuja katika nyanja nyingi na urembo una zama zake, hivyo kuwarejesha wananchi kutumia urembo asilia ni kazi kubwa ingawa urembo asili upo salama na hauna kemikali.

"Kwa dhama za sasa, ukiwaambia watu warudi katika urembo wa kujipaka maparachichi usoni au kutumia wanja wa kombe, itakuwa shida kwa sababu kwanza wafanyaji hawapo, wengi wameshafariki dunia na waliopo hawana ujuzi huo, sasa wana utaalamu mpya," alisema.

Ni kauli inayoungwa mkono na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho katika hospitali ya binafsi ya TASAKHATAA, Jualako Nassoro, anayesema ukubwa wa tatizo hilo unazidi kuongezeka huku wengi wa wanapopata madhara baada ya kubandika kope bandia, hawaendi hospitalini.

Kama ilivyodokezwa awali na wataalamu wenzake, Dk. Jualako anataja madhara ya kubandika kope bandia yanajumuisha macho kuwasha na kuvimba.

Anasema kope bandia huzisumbua kope asilia na kusababisha zing'oke ilhali zina umuhimu mkubwa katika ulinzi wa macho.

"Nimeshapokea wagonjwa waliopata madhara kutokana na kubandika kope bandia na wenyewe walinieleza kuwa chanzo cha macho kuuma ni baada ya kubandika kope. Kwa wastani ninapokea wagonjwa wawili walioathirika na tatizo hili kila mwezi.

"Kama watu wanaweza kujizuia kubandika kope bandia, ni jambo jema -- wasiweke kabisa ili kuepukana na madhara kwa sababu kila kiungo kina kazi yake na umuhimu wake katika mwili wa binadamu," anaonya bingwa huyo.

**WENYEWE WALONGA**

Baadhi ya wanawake waliozungumza na mwandishi wa habari hii, wanadai bila ya kubandika kope wakati wa sherehe, hawapendezi.

"Kwa kweli mimi bila kope bandi sitoboi (akiwa na maana hapendezi'. Asikwambie mtu, ukibandika kope huwa na mwonekano mzuri.

"Kiingiacho mjini si haramu, hivyo lazima tuendane na mabadiliko ya sasa katika suala la urembo, zikiwamo hizi kope za kubandika," anadai Zulfa Ali, mkazi wa mjini Unguja.

Kuhusu gharama za kope bandia, Zulfa anasema ni za wastani kutegemea na aina ya kope anayohitaji mtumiaji; kwa Unguja zipo za kuanzia Sh. 3,000 na hadi Sh. 10,000.

"Matumizi yake inategemea na utunzaji wako. Kama ukitunza vizuri, unaweza kuitumia hata mara tatu kwa kurudia," Zulfa anasema.

Fatma Hamad, mkazi wa mjini Unguja, anasema ameacha kutumia kope bandia baada ya kumletea madhara, hata kupelekwa hospitalini kupatiwa matibabu ya macho.

"Siku za mwanzo nilipoanza kubandika kope, sikuona madhara yoyote lakini baada ya mwaka mmoja, macho yangu yakawa yanawasha kama nimeweka pilipili na yakawa yanavimba na kutoa machozi.

"Nilipoona hali hiyo huku nikipata maumivu makali machoni, niliamua kufika katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya matibabu na ndipo niliposhauriwa na daktari kuacha matumizi ya kope bandia kwa sababu zina madhara," Fatma anasimulia na kubainisha kuwa alipona baada ya kupatiwa matibabu.

"Ni suala la kujiendekeza tu kusema kuwa bila ya kubandika kope huwezi kupendeza. Mimi ninakataa kwani kabla ya urembo wa kope haujaingia watu walikuwa hawapendezi," Fatma anahoji.

Raya Khamis mmoja ya wafanyakazi wa saluni mjini Unguja, anasema kuwa kwa mwezi hupamba maharusi watano hadi saba na wote hubandika kope kwa hiyari yao na wengine hutaka hadi kiini bandia cha jicho.

"Wateja wangu wanaokuja kupamba huwa ninawauliza 'je, unabandika kope?' Wengi wao husema 'ndio', na gharama za ubandikaji kope inategemea. Kama mteja nikimpamba mimi kwa kila kitu changu hadi kope, gharama yake ni Sh. 20,000 lakini bila ya kope ni Sh. 15,000," anasema mpambaji huyo.

Anaeleza kuwa kope bandia huenda sambamba na gundi, akisisitiza kuwa bila ya kutumia gundi kope haiwezi kukaa kwenye jicho.

Alipoulizwa kuhusu wateja wake kupata madhara kutokana na kubandika kope, Raya ana mrejesho huu: "Wapo ambao ukiwabandika kope wanatokwa na machozi, lakini wapo ambao wanapozitoa kope hizo hupata maumivu katika jicho."

**BINGWA MUHIMBILI**

Kukiwa na ushuhuda huo wa upambaji, Daktari Bingwa wa Macho katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Mloganzila, Yusta Mtogo, anaungana na matabibu wenzake kwamba ubandikaji kope bandia una madhara kiafya.

Dk. Yusta anasema wanaobandika kope bandia hutumia gundi ili kope hizo zikae vizuri kwenye macho, lakini gundi hiyo huleta uzio kwenye macho, macho kuwa mekundu, kuwasha, kutoa machozi au kuhisi kama kuna mchanga katika jicho.

"Madhara mengine ya kope bandia ni maambukizi kwenye macho, kwa sababu kope bandia zina nafasi ya kubeba vidudu hasa bakteria ambao wakiingia katika macho wanaweza kuleta maambukizi, hivyo mhusika kutokwa na tongotongo, machozi mengi, wekundu wa macho na maumivu ya macho na hata macho kuogopa mwangaza.

"Kope bandia zisipoweka vizuri, zinaweza kugeuka, na zikigeuka huleta mikwaruzo kwenye kioo cha jicho na kusababisha vidonda, hivyo ni muhimu anayetaka kuweka kope bandia awekewe na mtu mzoefu ili aziweke vizuri kupunguza madhara ambayo yanaweza kutokea.

"Matumizi ya muda mrefu ya kope bandia pia yanapelekea kope asili kudondoka na kung'oka, hivyo kope bandia zikitumika kwa muda mrefu kope asili zinaisha. Kope bandia zinaleta mwonekano mzuri lakini kope za asili zinaleta ulinzi wa macho dhidi ya vidudu, vumbi na majasho yasiingie machoni, hivyo kope za asili zikitoka zote, macho lazima yapate changamoto," bingwa huyo anaonya.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Mpango ufundishaji uraia, katiba waiva

Na Frank Monyo

SERIKALI iko katika hatua za mwisho kukamilisha mpango kazi wa ufundishaji wa elimu ya katiba na uraia katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi unaolenga kuongeza chachu ya uzalendo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Franklin Rwezimula, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akifungua kikao cha kujadili mpango kazi huo. Kikao hicho kimeandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wa elimu.

Alisema elimu hiyo itakuwa chachu ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii, kuongeza uzalendo katika mioyo na akili za wanafunzi, utii kwa Katiba ya Tanzania, kuimarisha umoja wa kitaifa, kukuza ushiriki wa kidemokrasia na kudumisha amani na utulivu nchini.

Pia alisema elimu ya katiba na uraia itasaidia kuandaa vijana wanaozingatia haki na wajibu wao kwa nchi yao ya Tanzania.

"Ni imani yangu kuwa elimu itakayotolewa kwa wanafunzi wa awali, msingi, sekondari na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi itawezesha kizazi kijacho kuwa chenye maadili, ujuzi, maarifa, wazalendo wa kweli na wenye kuipenda nchi yao.

"Hili ni jambo jema na la kuungwa mkono, kwani taifa linahitaji kizazi chenye uzalendo ili kuenzi na kudumisha amani ya nchi," alisema.

Alisema elimu hiyo ni muhimu kwa kizazi cha sasa kwa kuwa kuna changamoto kadhaa hususani uelewa mdogo wa uzalendo na maadili pamoja na misingi ya haki za binadamu.

"Suala hili likikamilika na elimu ya katiba na uraia ikianza kutolewa italeta chachu kwa taifa letu na kitasaidia kukamilisha malengo ya wizara ya utoaji wa elimu ya katiba na uraia kwa umma zikiwamo taasisi za elimu," alisema.

Kwa upande wa VETA, alisema tayari ziliundwa moduli za elimu zinazopendekezwa kujumuishwa katika muhtasari wa ufundishaji katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na zipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza kufundishwa Januari, 2025.

Alibainisha kuwa katika kikao hicho wadau hao watapitia mpango huo kuangalia maudhui ya katiba na uraia kulingana na silabasi za shule na vyuo hivyo.

Awali, alisema kikao hicho kilitanguliwa na vikao kazi vya wataalam wa wizara hiyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais – Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Taasisi ya Elimu Tanzania ambavyo vilitoa mapendekezo ya maudhui ya Elimu ya Katiba na Uraia yatakayofundishwa kuanzia elimu ya awali, msingi na sekondari sambamba na mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023.

Alisema kikao kingine cha pili kilijumuisha wataalam kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kwa lengo la kuunda moduli za elimu zinazopendekezwa kujumuishwa katika Mihutasari ya ufundishaji katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi.

"Kikao cha tatu kilijumuisha wataalam wa pande mbili za vikao vilivyotangulia na lengo lilikuwa kupata uelewa wa pamoja kuhusu Maudhui ya Elimu ya Katiba na Uraia na namna bora ya ufundishaji wa maudhui hayo.

"Kikao cha mwisho kiliwahusisha wataalam kutoka VETA na Chuo cha Mahakama Lushoto (IJA) ambacho kililenga kuchambua maudhui hayo ili kupata maudhui kuu na maudhui mahususi na kuandaa muhtasari wa kufundishia katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi," alisema.

Mtaalam Mwandamizi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Jerome Machuge, alisema wameona elimu hiyo ifundishwe sambamba na Somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, alisema katika mtaala wa ufundi stadi, vijana watafundishwa masuala ya Katiba na Uraia ili kuwa wazalendo na kujitambua kuilinda na kuitetea nchi yao.

Alisema elimu hiyo ni muhimu sana kwa vijana kwani itasaidia kuandaa vijana na jamii inayozingatia haki na wajibu na wenye kujua nini wanatakiwa kufanya na nini hawatakiwi kufanya ili kuilinda nchi.

# Waonywa kuwaachia mihuri ya ofisi wenza wao

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

WENYEVITI 155 wa vijiji, mitaa na vitongoji katika Manispaa ya Singida wamekula kiapo cha kuanza kazi rasmi huku wakitakiwa kuzingatia taratibu na sheria katika utendaji wa kazi.

Wameagizwa kuwa wanaposafiri wasiwe wanawaachia mihuri ya ofisi wake zao au waume zao.

Wenyeviti hao ambao wote wanatokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliapishwa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo Utemini, Ferdinand Njau na kushuhudiwa na Mkurugenzi wa Manispaa, Joanfaith Kataraia.

Katibu wa UWT Wilaya ya Singida Mjini, Naomi David, akizungumza na wenyeviti hao kabla ya kuapishwa alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wenyeviti wanaposafiri kuwaachia mihuri ya ofisi wenzi wao wake kitu ambacho ni kinyume cha utaratibu na sheria.

"Mwenyekiti ukisafiri mhuri wa ofisini muachie mjumbe si mke wako au mume wako. jambo hili kama chama hatutakubali kuona linajitokeza kwa sababu mambo kama haya yanasababisha malalamiko kutoka kwa wananchi wanaotaka huduma," alisema.

Naye Kataraia aliwataka wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji kuwa viongozi bora na wa mfano katika utendaji wao wa kazi na kuhakikisha hawamwangushi Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema viongozi hao wanalo jukumu la kuwahudumia wananchi vizuri katika maeneo yao na kuwa sauti za wananchi kwa kuhakikisha wanazipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

"Majukumu yenu ni pamoja na kuhakikisha mnasimamia mapato na matumizi, kusimamia usalana na amani katika maeneo yenu, kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yenu na kuitisha mikutano ya wananchi ambayo iko kwa mujibu wa sheria " alisema Kataraia.

Hakimu Njau aliwataka wenyeviti hao kufanya kazi kwa uaminifu na kutoa ushirikiano kwa viongozi wa serikali ili kuleta maendeleo ya haraka nchini.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA PILI WA JUMUIYA YA WAHASIBU WAKUU WA SERIKALI AFRIKA-AAAG

Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wahasibu wa Serikali wa Afrika mwaka 2024 (AAAG) utakaofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba, 2024.

Mkutano wa pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika utakuwa na mada mtambuka ambazo zitasaidia watumishi wa kada mbalimbali kuwaongezea ujuzi na Maarifa.

Pia Mkutano huu utasaidia Viongozi na Watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na Viongozi na Watumishi toka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na IMF. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ada ya ushiriki ya mkutano ni **Shilingi za Kitanzania 1,300,000/=** kwa kila mshiriki. Hivyo, Mamlaka husika zinaombwa kuwaruhusu na kuwalipia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Maafisa Usimamizi wa Fedha, Maafisa TEHAMA na watumishi wa kada nyingine kuhudhuria mkutano huu.

Washiriki wote wanatakiwa kuanza kijisajili kupitia lango (portal) lifuatalo: https://conference.aaag.org.zm kuanzia sasa hadi tarehe 01 Disemba, 2024 na ada ya ushiriki ilipwe kupitia **akaunti namba 9924915301 yenye jina African Association of Accountants General (AAAG).**

Aidha, kwa Taasisi za Umma, Kampuni mbalimbali na watu binafsi wanaotaka kudhamini Mkutano huu kwa lengo la kujitangaza kibiashara na kufanikisha Mkutano huu; Wizara ya Fedha inawakaribisha.

Kwa mawasiliano zaidi piga Namba ya simu +255 713 525 592 barua pepe, veronica.kishala@hazina.go.tz na evans.sayile@hazina.go.tz Sanduku la Posta ni Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha S.L.P 2802, Dodoma.

Pia kama muombaji amesahau namba ya simu, barua pepe na Sanduku la Posta anaweza kupata mawasiliano kupitia wakuu wa Hazina Ndogo waliopo kila mkoa Tanzania bara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Maandalizi Mkutano wa AAAG,**
**Wizara ya Fedha**
**Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Novemba, 2024**

218265202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia yaanzie katika familia

**MATUKIO** ya ukatili wa kijinsia yamekuwa yakiripotiwa kuongezeka mwaka hadi mwaka huku waathirika wakubwa wakiwa wanawake na watoto. Kutokana na kuongezeka kwa matukio hayo, serikali kwa kushirikiana na wadau yakiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari wamekuwa wakipaza sauti katika kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa na jamii inaishi katika hali ya usalama.

Hivi sasa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yanaendelea sehemu mbalimbali nchini. Maadhimisho hayo yaliyoanza Novemba 25 hadi Desemba 10, mwaka huu, yanabeba kaulimbiu "Miaka 30 ya Beijing, Tokomeza Ukatili wa Kijinsia".

Matukio hayo ya ukatili wa kijinsia, awali yalionekana kukithiri na kuongezeka katika mikoa kadhaa ambayo ilikuwa ikiripotiwa kufanya mauaji yanayodaiwa kuwa yanatokana na wivu wa mapenzi, vipigo kwa wanawake na ukeketaji. Lakini hivi sasa vitendo hivyo vimeenea kila mkoa huku ikielezwa kuwa Iringa ndiyo inayoongoza ikifuatiwa na Manyara.

Ripoti za hivi karibuni zinaonesha kuwa katika mkoa wa Manyara kuna kasi ya ongezeko la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, baada ya kuripotiwa matukio 7,893 katika kipindi kisichozidi miezi 10. Ripoti ya Hali ya Afya na Demografia Tanzania (TDHS), inaonesha kuwa chanzo cha ukatili huo, asilimia 60 unatokea ndani ya familia na asilimia 40 ni ule unaotokea shuleni.

Akizungumza wakati wa wa uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili mkoani Manyara, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa, Anna Fisoo, alisema ukatili huo ulioripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka huu, unaonesha kuwa ulawiti siku hizi umekuwa fasheni katika jamii. Sababu kubwa ya kuenea kwa aina hiyo ya ukatili ni wazazi kukosa umakini kwa watoto kwa sababu wengi wao kujikita katika majukumu ya kila siku, vikoba na kutafuta pesa.

Licha ya jitihada zinazofanyika za kukomesha vitendo hivyo, kumekuwa na taarifa za kuongezeka katika mikoa mbalimbali, vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti kila uchao kwa baadhi ya wanaume kuwapiga wenza wao hatimaye kuwasababishia ulemavu wa viungo na hata vifo. Katika baadhi ya maeneo pia imekuwa ikiripotiwa baadhi ya wanaume kuwapiga na kuwaua wake zao pamoja na watoto kwa madai kwamba vipimo vya vinasaba (DNA) vineonesha kuwa si watoto wao.

Pamoja na wivu wa kimapenzi, ukatili huo pia umejikita katika unyanyasaji wa kijinsia sehemu za kazi kwa baadhi ya wafanyakazi kulazimishwa kushiriki vitendo vya ngono. Wanaokataa kufanya hivyo, hufanyiwa visa na kufukuzwa kazi au kuamua kuacha kazi.

Pia ukeketaji bado ni tatizo sugu katika baadhi ya mikoa na jambo hilo hufanyika kwa siri na wahusika wamekuwa wakibadilisha mbinu na staili za kutekeleza ili kukwepa mkono wa dola.


Tatizo la ukatili wa kijinsia kwa sasa linaonekana kuzidi kuota mizizi licha ya kuwapo kwa kampeni mbalimbali na kwa muktadha tofauti. Kwa mantiki hiyo, nguvu zaidi inahitajika katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa hatimaye Tanzania kuwa huru dhidi ya matukio kama hayo. Vita dhidi ya ukatili wa kijinsia haiwezi kufanikiwa iwapo kila mmoja hatashiriki kikamilifu kuibua, kuripoti na kuchukua hatua.

Katika moja ya kampeni za kupambana na kutokomeza UKimwi, kuna msemo kwamba 'it begins with you' kwa maana kwamba inaanza na wewe. Vivyo hivyo, vita dhidi ya ukatili wa kijinsia vinapaswa kuanza na mtu mmoja mmoja, familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yamekuwa mstari wa mbele, yanapaswa kutoa mwongozo au kuongoza mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa kuhamasisha jamii kushiriki kuanzia ngazi ya familia.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele, juzi aliyaagiza mashirika hayo kuhamishia kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia katika ngazi ya familia kutokana na vitendo hivyo kukithiri katika wilaya hiyo, hivyo ni wajibu wa mashirika kuhakikisha familia zinahusishwa moja kwa moja ili kufikia kilele cha mafanikio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Enyi wana- Rufiji, kinachoendelea kuhusu korosho yetu hiki hapa



Na Yasmine Protace

**KATIKA** jamii mara zote wanasema kizuri kula na nduguyo. Kujua vyema, kwetu wenye unasaba na mkoa wa Pwani, safari ikisonga hadi Kusini mwa nchi, suala la zao la korosho linahusika moja kwa moja na uchumi wetu.

Ngoja niwape mchapo wa kinachoendelea kuhusu korosho ya Pwani, ambayo 'juzi kati'nilikuwa na watoa uamuzi, hebu tufuatane, ujue kinachoendelea kuhusu korosho yetu Pwani:

Ni mnada wa sita wa korosho katika mkoa wa Pwani ambako korosho hizo daraja la kwanza bei ya kuuzwa ilipangwa kuuzwa kwa Sh. 2720 kwa kilo.

Hata hivyo pamoja na kutangazwa kwa bei hiyo, hakuna wanunuzi waliojitokeza kununua kwa bei hiyo na wanunuzi walijitokeza kwa kununua kwa bei ya shilingi 2666.71.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Mkoa wa Pwani - CORECU mkoa wa Pwani Hamis Mantawela, anasema kuwa mnada wa kwanza hadi wa nne asilimia kubwa ya wakulima imeishalipwa pesa zao na wanaodai ni wakulima wachache.

Anasema zaidi ya shilingi bilioni 60 zimelipwa katika minada minne, akisema:"huu ni mnada wa sita,kiasi cha Sh.bilioni 60 kimelipwa katika minada minne," anasema.

Anaongeza kuwa baadhi ya wakulima ambao hawajalipwa katika mnada wa kwanza ni namba za simu kuwa tofauti na majina yao huku wengine kadi zao za benki zikiwa hazifanyi kazi kwa muda mrefu.

Mantawela anasema kuwa wakulima waendelee kupeleka korosho katika vyama vya msingi ili waweze kunufaika na fedha ambazo watazipata.

" Mnada unakaribia kuisha hivyo inatakiwa wakulima waendelee kupeleka korosho katika vyama vya msingi,endapo korosho wataziacha nyumbani mnada ukiisha watakaopata hasara ni wakulima," anasema.

Anaongeza kuwa kwa wale wakulima ambao hawajapata mnada wa kwanza hadi wa nne wanatakiwa kwenda kwa wenyeviti wa vyama vyao vya msingi ili wakatoe taarifa zao ili ziweze kufanyiwa kazi.

> **" Mnada unakaribia kuisha hivyo inatakiwa wakulima waendelee kupeleka korosho katika vyama vya msingi,endapo korosho wataziacha nyumbani mnada ukiisha watakaopata hasara ni wakulima," anasema.**

Pia anawataka wakulima wanapopeleka korosho katika vyama vya ushirika, wabebe na kadi zao za benki ili kuondoa sintofahamu katika malipo.

Akizungumzia bei ya korosho kushuka kutoka zaidi ya shilingi elfu tatu hadi Sh.2,600 kwa kilo daraja la kwanza, anasema kuwa minada kila mwaka huwa inabadilika bei minada yote huwezi kuuza mnada wa kwanza hadi wa mwisho bei ni moja.

" Mnada wa kwanza hadi wa tatu bei daraja la kwanza kilo iliuzwa zaidi ya shilingi 3000, lakini mnada wa nne, hadi wa sita bei ya korosho imekuwa zaidi ya shilingi 2000 kwa kilo moja ya daraja la kwanza," anatamka.

Anasema bei hiyo siyo mbaya ikilinganishwa na bei za miaka mitatu ya nyuma, huku akizungumzia uchache wa magunia katika ghala la Rufiji, kwamba walitarajia kupata magunia 50,000 lakini wamefanikiwa kupata magunia 30,000. Mantawela anasema kuwa chama ambacho kinamagunia kiviazime vyama vingine ili waweze kuweka korosho na kwamba makabidhiano yafanyike ili kuhakikisha waliokuwa na magunia vyama vyao vihakikishe vinarudisha. Pia, anataja kwamba katika mnada wa sita korosho za Rufiji kilo moja daraja la kwanza zimeuzwa kwa Sh. 2666.71 huku daraja la pili zikiuzwa kwa Sh. 2364.50.

Wilaya ya Kibiti, daraja la pili zimeuzwa kwa shilingi 2300; wilaya ya Mkuranga korosho daraja la pili zimeuzwa kwa Sh. 2220.

Jumanne Uwelo, Mwenyekiti wa Amcoss anasema kuwa utaratibu ufanywe katika maghala,ambapo changamoto wanayokutana nayo ni kukaa katika maghala zaidi ya wiki ukisubiri kushushwa kwa korosho.

Anasema maghala kuwa na foleni ya kupokea korosho nayo ni changamoto.

## HABARI KITAIFA

# SGR yaingiza Bil 28.5/- miezi mitano

**Na Jenifer Gilla**

TRENI ya Umeme ya Kisasa (SGR) imeingiza Sh. bilioni 28 tangu ilipoanza kutoa huduma ya usafiri Julai 14, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, aliyasema hayo juzi, baada ya kutembelea Stesheni ya Samia jijini Dodoma, kukagua shughuli za utoaji huduma za usafiri huo.

Alisema tangu mradi huo uanze kazi rasmi Julai, mwaka huu umeonesha manufaa makubwa kiuchumi kwa kusafirisha abiria 1,029,540 walioingiza zaidi ya Sh. bilioni 28.5.

"Tangu tumeanza huduma ya usafiri wa SGR tumeingiza Sh. 28,507,088,80, ni mafanikio makubwa huku matumizi yetu ya umeme yakiwa chini ya asilimia 10," alisema.

Aidha, Prof Kakyarara alitoa onyo kwa atakayebainika kuhujumu miundombinu pamoja na treni ya SGR kuwa hawatamvumilia na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria.

Aliwasihi Watanzania kila mmoja kuwa mlinzi wa miundombinu hiyo kwa kuwa ni uwekezaji ambao matokeo yake yanalinufaisha taifa na kuleta maendeleo ya wananchi.

"Miundombinu hii ni yetu sote,inalindwa kwa sheria kali za reli na ile ya uhujumu uchumi. Tutazitumia ipasavyo kulinda huu mradi wa Watanzania," alisisitiza.

**SAFARI**

Tangu kuanza kazi kwa mradi huo, umepitia changamoto mbalimbali ikiwamo hitilafu ya mifumo ya umeme ambayo imesababisha kusitisha safari zake mara kwa mara.

Tukio la aina hiyo lilitokea Agosti mosi, mwaka huu kwa treni hiyo ikiwa imebeba wageni mbalimbali waliotoka kushuhudia uzinduzi wa SGR Dodoma, ikikwama kwa saa kadhaa katika Stesheni ya Mkata, mkoani Morogoro.

Tukio kama hilo pia lilitokea Oktoba 10, mwaka huu na kusababisha abiria 1,417 na wafanyakazi 30 wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kukwama zaidi ya saa 30 kwenye stesheni ya Dodoma baada ya mabehewa mawili ya treni ya mizigo kuanguka eneo la Makutupora na Saranda Mkoani Singida.

Aidha, Novemba 3, mwaka huu TRC ililazimika kuomba radhi kwa abiria baada ya treni zake mbili za SGR kusimamisha safari kutokana na hitilafu iliyotokea katika mifumo ya uendeshaji.

Julai 2, mwaka huu TRC ilisema hitilafu ya umeme iliyosababisha Treni ya SGR kutoka Dar - Dodoma kusimama katika Stesheni ya Kilosa na Kidete na taarifa ilisababishwa na ngedere au bundi waliogusa nyaya za umeme zilizotandazwa juu ya reli.

Shirika hilo pia liliripoti kuwapo watu wanaohujumu miundombinu ya reli kwa kuiba na nyaya za shaba kwa lengo la kujipatia fedha.

Novemba 12, mwaka huu, Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma lilitangaza kuwashikilia watuhumiwa wawili, Said Sempinga (39) na Michael Robert (44), wakazi wa Kilosa, mkoani Morgoro kwa tuhuma za kukata na kuiba waya wa shaba (copper wire) kutoka katika madaraja matatu ya reli hiyo.

Lilisema pia linawashikilia watuhumiwa wanne kwa tuhuma za kukata nyaya za shaba katika mradi wa treni ya umeme SGR Wilaya ya Bahi.

Novemba 25, mwaka huu Jeshi la Polisi pia liliwashikilia watoto wawili wenye umri wa miaka 12 na 16 kwa tuhuma za kurusha mawe na kuvunja vioo viwili vya treni ya mwendokasi katika Kijiji cha Manase, wilayani Chamwino.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, DCP David Misime, alisema watoto hao walirusha mawe wakati treni hiyo inapita ikitokea jijini Dar es Salaam kwenda Dodoma Novemba 22, mwaka huu.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Franklin Rwezimula (kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kikao maalum cha kupitishwa kwa mpango kazi wa ufundishwaji wa Elimu ya Katiba, Sheria na Uraia mashuleni. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Anthony Kasole. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Shahidi huru kesi kusafirisha dawa abanwa kwa maswali

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI Tumaini Mgonja anayemtetea Samweli Kagisha na mkewe Brigette Uwela, wanaoshtakiwa kwa kusafirisha dawa za kulevya amembana kwa maswali shahidi huru, akidai amekuwa anatoa ushahidi katika kesi nyingi za dawa za kulevya kama hakuna watu wengine maeneo ya Posta.

Hayo yaliibuka jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Isaya Arufani, wakati Julius Mazimu akitoa ushahidi.

Shahidi huyo ambaye ni huru alidai kuwa, Januari 31, mwaka huu alifuatwa na Koplo Jackson akashuhudie ufungaji wa vielelezo cha unga unaodhaniwa kuwa dawa za kulevya, katika chumba aliwakuta watu watatu na Jackson alimtambulisha kwao.

Aliwataja watu hao kuwa ni Inspekta Johari, Samweli na Brigette na baada ya utambulisho Johari alitoka nje na aliporudi alikuwa kashika bahasha ya kaki. Anadai alishuhudia kielelezo hicho kikifungwa na kupelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi.

Wakili Mgonja akiwawakilisha wateja wake alimtaka shahidi aieleze mahakama ni mara ngapi Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wamemtumia kushuhudia ufungaji wa vielelezo.

Mgonja alidai jina la Julius Mazimu ni maarufu katika kesi nyingi za dawa za kulevya na kwanini wasitumiwe watu wengine wakati maeneo ya Posta watu ni wengi wakiwamo wapita njia.

Akijibu, Mazimu alidai ameshatumiwa na mamlaka katika kesi mbili na hajui kwanini anatumiwa yeye.

Alidai anafanya kazi ya usafi katika jengo la Utumishi na kuongeza kwamba katika hilo jengo hayupo peke yake kuna watu wengine.

Shahidi alidai katika chumba cha kufungia vielelezo hakuona mtoto mdogo wa mshtakiwa Brigette na kwamba vielelezo alivyoshuhudia ulikuwa unga na chenga chenga.

Shahidi mwingine wa sita, Inspekta Johari Msirikale, alidai alipokea vielelezo mbalimbali akavipa namba A hadi H na alitaja kuwa ni simu, hati ya kusafiria ya Rwanda, Kitambulisho cha Taifa vyote vya Brigette na cheti cha kuzaliwa cha mshtakiwa Samweli.

Inspekta Johari alidai alifunga kielelezo cha unga na chenga chenga huku washtakiwa walishuhudia na kumpa Koplo Jackson akipeleke Ofisi ya Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi na ilibainika ilikuwa dawa za kulevya aina ya heroine.

Washtakiwa walikamatwa wilayani Mkuranga Januari 30 mwaka huu wakituhumiwa kujihusisha na biashara ya kusafirisha dawa za kulevya.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Madaktari bingwa 20 waenda Comoro kutoa matibabu

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa 20 kutoka hospitali kubwa nchini wamesafiri kwenda nchini Comoro kwa ajili ya kuweka kambi ya wiki moja ya uchunguzi na utoaji huduma za kibingwa za magonjwa mbalimbali ikiwamo upasuaji wa moyo, saratani na ubongo.

Madaktari hao wanatoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Mifupa (MOI) na Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma.

Akizungumza jana kabla ya madaktari hao kuondoka, Mratibu wa Utalii Tiba kutoka Wizara ya Afya, Dk. Aisha Mahita, alisema Tanzania imekuwa ikipokea wagonjwa wengi kutoka nchini Comoro ndio sababu wameamua kwenda kuweka kambi ya matibabu ili kuona magonjwa gani yanayowasumbua na kuyawekea mkakati.

"Tunakwenda kutangaza utalii tiba serikali yetu imewekeza kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya, tuna mambo mengi sana yamefanyika kwa hiyo lazima dunia ijue kwamba kwenye sekta ya matibabu Tanzania iko vizuri na baada ya Comoro tutakwenda nchi zingine," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba, Abdulmalik Mollel, alisema lengo la safari hiyo ni kuwajengea uwezo madaktari wa Comoro na kuangalia fursa za uwekezaji sekta ya afya zilizopo nchini humo.

"Nina furaha kumwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba Kitaifa, Profesa Mohamed Janabi kwasababu madaktari kutoka hospitali zetu kubwa kwa usaidizi wa Wizara ya Afya na tutaangalia wadau ambao tunaweza kufanya kazi nao na tutaangalia fursa zilizopo kule na kushauriana na mamlaka husika kuona namna ya kuzitumia," alisema Mollel.

Aliwashukuru wakurugenzi wa hospitali zote zilizotoa madaktari bingwa kwenda kutoa huduma nchini humo na pia Mkurugenzi wa JKCI, Dk. Peter Kisenge kwa kuwa ndiye mratibu mkuu wa safari hiyo.



Mratibu wa Utalii Tiba wa Wizara ya Afya, Dk. Aisha Mahita (katikati), akizungumza katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Terminal III, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kuuaga ujumbe wa madaktari bingwa 20 kutoka hospitali mbalimbali nchini, walioondoka kwenda Comoro kutoa huduma za kibingwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

"Sehemu kubwa ya mafanikio haya ni uratibu wa Dk. Kisenge kwasababu yeye ndiye amewasiliana na wakurugenzi wenzake wa hospitali zilizotoa madaktari bingwa kwa hiyo sisi Kamati ya Utalii Tiba tunamshukuru kwa kazi kubwa ambayo ameifanya," alisema Mollel.

Pia, aliushukuru ubalozi wa Tanzania nchini Comoro kwa kufanyakazi kubwa kushirikiana na Kamati ya utalii tiba kufanikisha safari hiyo.

Daktari bingwa wa moyo kutoka JKCI, Salehe Hamis, alisema watafanya matibabu mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa saratani, mifupa, ubongo na moyo ili kuendeleza utamaduni wa kutoa matibabu ya afya kwenye nchi jirani.

"Umekuwa utamaduni wa JKCI kutoa huduma za kibingwa kwenye mikoa mbalimbali nchini na sasa tumeanza kwenda nchi za jirani kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye upande wa teknoljia na vifaa vya kisasa na safari hii tuna wataalamu kutoka hospitali mbalimbali," alisema Dk. Hamis Daktari bingwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kutoka MOI, Zarina Ali, alisema watawajengea uwezo madaktari wa nchi hiyo ili waweze kutibu magonjwa ya kawaida ya ubongo na mishipa ya fahamu na kwa yale watakaokuwa wanashindwa wanawaleta wagonjwa kwenye taasisi ya MOI.

"Tutatoa huduma za ubongo, mishipa ya fahamu na ubongo kama sehemu ya kuhamasisha utalii tiba nchini Tanzania na tutashirikiana na wataalamu wa tiba mbalimbali kwa wiki nzima tukiwa kule," alisema.

Daktari bingwa wa saratani kutoka Ocean Road, Mark Athumani, alisema kambi hiyo ya matibabu ya wiki moja itasaidia kuongeza uhusiano wa nchi hizo mbili.

"Kwenye msafara huu Ocean Road imepeleka wataalamu saba wakiwamo madaktari bingwa watano na watalamu wawili wa uchunguzi wa awali wa maradhi ya saratani kwa hiyo kule tutatoa uchunguzi wa uvimbe mbalimbali," alisema na kuongeza;

"Tutatoa matibabu mbalimbali ya kuwakinga wanawake wasipate saratani ya mlango wa kizazi na saratani za matiti, ngozi na tezi dume na tutatoa pia elimu ya namna ya kujikinga na saratani. Serikali yetu imewekeza sana kwenye tiba ya saratani na kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na kati sisi ndio wenye mashine bora kabisa ya uchunguzi wa saratani," alisema.

# TARURA yatengewa mamilioni matengenezo barabara

**Na Jumbe Ismailly,**
MKALAMA

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida umetumia Sh. milioni 224 kuifanyia matengenezo ya muda maalumu barabara ya Iguguno-Lyelembo-Msingi yenye urefu wa kilomita 4.3 na ujenzi wa madaraja mawili ya mawe.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Rahabu Thomas, amesema mradi huo uliopo katika vijiji vya Kidi na Yulansoni, Kata ya Msingi, ulianza kutekelezwa Septemba 20, mwaka jana na kukamilika Machi 18, mwaka huu.

Mhandisi Rahabu alisema mradi huo uliotekelezwa na Mkandarasi M/S Timajo Engineering Company Limited yenye makao yake makuu Makambako, uliogharamiwa na serikali kuu kupitia fedha za tozo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 kwa gharama ya Sh. 224,122,220.

Meneja wa Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Singida, Mhandisi Ibrahimu Kibasa, alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 TARURA Mkoa wa Singida ilitengewa bajeti ya Sh. bilioni 24.5.

Fedha hizo zilikuwa katika makundi matano ambayo ni fedha za matengenezo ya kawaida (ukarabati) Sh. bilioni 5.5, fedha za maendeleo, Sh. milioni 600, fedha za Mfuko wa Jimbo Shiling bilioni nne, fedha za ushuru wa mafuta Sh. bilioni 12 na za kuondoa vikwazo Sh. bilioni 1.8.

# Wabunifu waja na mfumo mafao kwa bodaboda

**Na Maulid Mmbaga**

WABUNIFU wa masuala ya sayansi na teknolojia ambao wameendelezwa chini ya atamizi ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), wamekuja na bunifu zinazoleta suluhu za kijamii ikiwamo mfumo mahususi kwa ajili ya kuwasaidia madereva bodaboda kuwa na mfuko maalumu wa kuhifadhi akiba itakayowasaidia baadaye.

Akizungumza na Nipashe siku chache zilizopita mkoani Dar es Salaam, Jastine Kashegera, ambaye ni miongoni mwa wabunifu hao, alisema sekta hiyo ya usafirishaji imeajiri kiasi kikubwa cha vijana nchini na kwamba mfumo huo pia utawasaidia kuongeza kipato chao kutoka wastani wa Sh. 10,000 hadi 50,000 kwa siku.

Alisema mfumo huo utawasaidia madereva kupata abiria pamoja na kuwaunganisha na wadau mbalimbali ambao watakuwa na uhitaji wa huduma ya usafiri na kwamba hatua hiyo itawaongezea mzunguko wa kifedha na kuifanya kazi hiyo kuwa na tija zaidi.

"Moja ya shida kubwa inayowakabili madereva wa bodaboda ni kutokuwa na utaratibu maalumu wa kujiwekea akiba ambayo itawasaidia baadaye kama kiinua mgongo, lakini ubunifu huu utamuwezesha dereva kila fedha anayopata kuna kiasi kitakuwa kinaingia kwenye mfuko wake maalumu kwaajili ya matunzo ya baadaye.

"Hadi sasa kuna zaidi ya madereva 5,000 ambao wamejiunga na mfumo huu ambao unafanyakazi mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya, na sasa tunajaribu kusambaa katika miji zaidi ya 20 ambayo haina huduma ya usafiri, na tunatarajia mfumo huu utaenda kutumika kwa zaidi ya vijana milioni mbili," alisema Kashegera.

Aliongeza kuwa hiyo ni sekta ambayo imeajiri asilimia kubwa ya vijana kuliko nyingine yoyote, kwahiyo wametengeneza kitu cha kibunifu ambacho wanaamini kitasaidia vijana wenzao wasifanye kazi tu ila wawe na utaratibu maalumu ambao utawawezesha kuishi vizuri hata baada ya kustaafu kazi hiyo.

Aidha, aliishukuru COSTECH kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kuendeleza bunifu zao ambazo wana matumaini kwamba zitaenda kujibu changamoto zinazoikabili jamii na taifa kwa ujumla.

Erasto Mlyuka, Msimamizi wa Atamizi COSTECH, alisema tume hiyo inaibua wabunifu hao na kuwaweka katika hatua ambayo wanaweza wakaaminika na kupata uwezeshaji kutoka kwa wadau mbalimbali.

Alisema hadi sasa wameshakuwa na 'Incubation' atamizi kwa zaidi ya kampuni 45, na kati ya hayo ambayo yako ndani ni tisa, na yameweza kutengeneza ajira mbalimbali.

"Sisi tunasaidia ukuaji wa biashara za kibunifu kutoka hatua ya wazo hadi kuwa na kampuni ambayo itaenda kufanya kazi kwenye jamii, wakiwa kwenye atamizi wanahitaji vifaa na miundombinu mbalimbali itakayowasaidia kutoa kitu cha kiushindani ambako kwa sasa tunatumia vya vyuo vikuu.

"Vingine vya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), hivyo ndivyo tunavyoibua makampuni na kwa sasa yako 45, na kati ya hayo zaidi ya 10 yanafanya kazi kitaifa na kimataifa," alisema Mlyuka.



# Mbaroni tuhuma kumbaka mtoto wake

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JESHI la Polisi mkoani Manyara limemtia mbaroni, Paschal Lori, mkazi wa Negamsi, Kata ya Bagara katika Mji wa Babati, akikabiliwa na tuhuma ya kumbaka mtoto wake mwenye umri wa miaka minane.

Mtoto huyo (jina limehifadhiwa), ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili, alikutwa akiingiliwa kimwili na baba yake aliyekuwa amelewa.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Ahmed Makarani, akizungumzia tukio hilo alisema wanamshikilia Lori kwa mahojiano na ushahidi ukikamilika atafikishwa mahakamani.

Aidha, mke wa mtuhumiwa huyo, aitwaye Paskalina Tarimo, alisema mumewe alimbaka mtoto huyo Novemba 23 mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni nyumbani kwake.

"Nilikuwa nimekaa nje, nilimtuma ndani mtoto, baba yake alikuwa amelala. Nilipoona anachelewa kurudi nje, nilimfuata ndipo nilimkuta kitandani na baba yake wote wakiwa uchi.

Nilimhoji mtoto, akasema baba yake alikuwa akimpatia fedha shilingi 1,000 au shilingi 500 kwa wiki, akimwambia asimueleze mama yake; na mtoto alimweleza baba yake amekuwa akimfanyia hivyo."

Mama huyo, anasema alipomhoji mume wake kuwa wanafanya nini mume wake alimjibu tunafanya kile atakachofanya ukubwani.

Kwa mujibu wa mama huyo, mtuhumiwa ambaye ni mumewe, aliondoka nyumbani asubuhi siku hiyo na kurudi saa 6:00 mchana akiwa amelewa.

Baada ya tukio hilo mama huyo alitoa t aarifa Kituo Kikuu cha Polisi Babati na kupewa fomu namba tatu (PF3), ili aende Hospitali ya Mji wa Babati (Mrara), na alipoenda daktari alithibitisha kuwa mtoto ameingiliwa ila hakuna mchubuko na damu yoyote.

**"Nilikuwa nimekaa nje, nilimtuma ndani mtoto, baba yake alikuwa amelala. Nilipoona anachelewa kurudi nje, nilimfuata ndipo nilimkuta kitandani na baba yake wote wakiwa uchi.**




Mwanasheria wa shirika lisilo la kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Eliakim Paulo akizungumza wakati akihamasisha jamii kupiga vita ukatili, wakati wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia katika Kanisa la FPCT Galilaya, mtaa wa Maisaka, mjini Babati, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanaharakati wawashangaa wagombea S/mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAHARAKATI na wafeminia 15 wanaopinga rushwa ya ngono mkoani Kilimanjaro wameshangazwa na namna vyama vya siasa na wagombea kushindwa kueleza madhara ya rushwa ya ngono, walipokuwa katika majukwaa.

Wakizungumza juzi katika Mji wa Moshi, wakati wa kikao kazi cha siku 16 za kupinga ukatili kilichoandaliwa na shirika la KWIECO, Mariam Nduka, alisema katika majukwaa ya kampeni hakuna mgombea wala kiongozi aliyethubutu kuzungumzia rushwa ya ngono kwenye majukwaa na kuikemea sehemu mbalimbali.

Kikao kazi hicho kiliwajumuisha wanaharakati kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali, Jukwaa la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (TAPO) na wasaidizi wa kisheria.

"Rushwa ya ngono inakuwa ni siri sirini. Unakuta hata wale wenye kampeni wenyewe ni watu wanaweza kudai rushwa ya ngono kwa wale wanaokwenda kupiga kampeni. Hapa tunaongelea rushwa ya ngono, lakini tukitoka nje, hatuwezi kwenda kuliongelea hilo jambo, hata tunapokuwa kwenye yale majukwaa hatutamkagi kitu," alisema.

Honoratha Nasuwa, Mkurugenzi wa Programu wa NAFGEM, alisema watu sasa hivi hawana tena uwoga kuhusu rushwa ya ngono kwenye siasa, shuleni na ofisini.

"Naona kama mmomonyoko wa maadili na ukimya wa jamii, umekuwa kisababishi kikubwa sana kwa yule asiyetaka kufanya rushwa ya ngono, anafanya kutokana na ile faragha inayotengenezwa na wale wahitaji," alisema na kuongeza.

Kabla ya uchaguzi lazima ujipendekeze na kujipendekeza kwako inategemea unakutana na nani. Rushwa ya ngono inatembea kwa wale ambao ni wahamasishaji na hasa yale makundi yanayofanya kampeni usiku na wanakutana na vijana na kama yuko mwenye uwezo kiuchumi wanapatia hapo fursa.

Alisema kwenye siasa ndiko watu wanajiandaa sana wanajua kabisa pale ndio kuna fursa nitakutana na watu fulani, nitakutana na kila mtu. Kwa hiyo kila msichana amejiandaa na ukiangalia tu kwenye vyama vyote utakuta wamejiandaa.

Mwanasheria na mwasisi wa Shirika la KWIECO, Shamsa Namtula, akizungumzia rushwa hiyo ya ngono, alisema Sheria ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) ya Mwaka 2007 imeweka adhabu kali kwa kosa hilo. Kwa mujibu wa Veronica Ollomi wa Shirika la KWIECO, Februari mwaka 2022, wanawake zaidi ya 40 ambao ni watetezi wa haki za binadamu kutoka katika mashirika, asasi za kiraia na vikundi vya kijamii, waliingia makubaliano ya kuyafanyia kazi pamoja mambo manane, hasa rushwa ya ngono.

Septemba mwaka huu, Bunge lilipitisha Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya TAKUKURU ya Mwaka 2024, likiongeza wigo wa ukomo wa adhabu kwa waomba rushwa ya ngono kutoka miaka mitatu hadi 10, na faini ya Sh. milioni tano hadi 10.

# Wadau nishati kukutana kujadili upotevu wa umeme

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

JIJI la Arusha limeteuliwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa kikanda wa matumizi bora ya nishati, utakaowakutanisha wadau 400 wakiwamo mawaziri, wataalam na sekta binafsi.

Pamoja na mambo mengine mkutano huo utatumika kubadilishana uzoefu na uelewa katika masuala ya nishati, fursa zilizopo na uwekezaji.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Innocent Luoga, mkutano huo utafanyika kati ya Desemba 4 hadi mwaka huu, chini ya ufadhili wa programu ya pamoja ya Serikali ya Tanzania, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) na ubalozi wa Ireland.

"Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya, UNDP na Ubalozi wa Ireland, imeandaa mkutano wa kikanda kwa nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), unaohusu masuala ya matumizi bora ya nishati.


...Mkutano huo ujulikanao kama Regional Energy Efficiency Conference (REEC), mgeni rasmi atakuwa ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko."

Mhandisi Luoga, alisema mkutano huo una umuhimu mkubwa nchini kwa kuwa unahusisha matumizi ya umeme kwa ufanisi na kwa ubora, unalenga kupunguza upotevu wa umeme, kupunguza gharama za umeme na kulinda mazingira.

Aidha, alisema kuhusu utekelezaji na faida za programu hiyo, Tanzania tayari imeshaandaa mkakati wa matumizi bora ya nishati wa miaka 10 (2024-2034), ambapo hivi sasa serikali imeweka ufadhili wa wanafunzi wa kike katika masuala ya nishati.

Vilevile, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), limeshaanza kuandaa viwango vya matumizi bora ya nishati kwenye vifaa mbalimbali kama majokofu na wako vijana 152 ambao wamepata ufadhili kutokana na ubunifu katika matumizi bora ya nishati.

Programu Meneja wa Miradi ya Nishati kutoka EU, Massimiliano Pedretti, aliipongeza Tanzania kwa utekelezaji wa programu hiyo, ambayo imeonesha mafanikio makubwa, huku akieleza kuwa umoja huo utaongeza muda wa utekelezaji wa programu hiyo nchini.








Mkurugenzi wa shirika linahudumia waraibu wa dawa za kulevya la Life & Hope Rehabilitation Organization (LHRO), Al-karim Bhanji (kushoto), akizungumza mjini Bagamoyo, mkoani Pwani jana, katika mkutano wa kutoa taarifa ya kuhitimisha mradi wa kuiwezesha jamii ya waraibu wa dawa za kulevya kujua haki zao za msingi ulioendeshwa na shirika hilo kwa kipindi cha mwaka mmoja, kwenye wilaya tano za mkoani humo. Kutoka (kulia) ni Kaimu Mkuu wa Kituo cha Polisi Bagamoyo, Tumaini Mgobela, Kaimu Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bagamoyo, Veronica Salala na Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Kandi Lussingu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima tumbaku walia kukatwa fedha bila ridhaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku wa Chama cha Msingi Uyogo kilichopo Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameitaka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kurejesha Sh.milioni 51.784 walizokatwa kimakosa kwa kipindi cha misimu miwili.

Pia, wametishia kutoendelea kufanyakazi na benki hiyo kama fedha zao hazitarejeshwa ndani ya msimu huu.

Mwenyekiti wa chama hicho, Maganga Masanja alibainisha hayo juzi katika mkutano mkuu wa mwaka wa 31 uliohudhuriwa na wanachama 159 kati ya 179.

Mkutano huo ulilenga kujadili masuala mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa pembejeo za ruzuku, viuatilifu, mapato na matumizi pamoja na hali ya uzalishaji wa mazao ya kibiashara tumbaku na pamba.

Alisema wamekatwa fedha kimakosa zaidi ya Sh.milioni 51.784 na walipofuatilia waliambiwa zimekatwa kwa ajili ya bima ya mazao ambayo hawakuiomba wala kuitaka.

Hivyo walimtaka Meneja wa Benki hiyo Simon Mtwale kuhakikisha anazirejesha na kama asipofanya hivyo hawataendelea kufanyakazi na benki hiyo kwa sababu watakuwa wanawaingiza hasara kwenye uzalishaji.

Masanja alisema, msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24 walikatwa Dola za Marekani 8,024 sawa na Sh.milioni 21.263 huku msimu huu wa 2024/25 wakikatwa Dola za Marekani 11,346 sawa na Sh.milioni 30.263.

> **Mmoja wa wakulima, Andrew Kasala alisema kukatwa fedha bila taarifa na taasisi za kifedha bila mpango ni njia mojawapo ya kuwadidimiza wakulima wasiendelee kukua.**

Alisema fedha hizo wangeweza kuzitumia kwenye maandalizi ya kilimo na kuondokana kuingia kwenye mikopo na benki hiyo.

Mmoja wa wakulima, Andrew Kasala alisema kukatwa fedha bila taarifa na taasisi za kifedha mpango ni njia mojawapo ya kuwadidimiza wakulima wasiendelee kukua. Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Ushetu, Fadhili Mwamalili alisema taasisi za kifedha zinazofanya kazi na wakulima wa tumbaku na pamba wazingatie maombi wanayopokea kutoka kwa wateja wao.

Alisema suala la bima ya mazao siyo lazima na kushauri kurejesha fedha hizo ili kuondoa malalamiko yasiyokuwa ya lazima baina yao na wakulima wao.

Akijibu tuhuma hizo, Meneja wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) Tawi la Kahama, Simon Mtwale alikili fedha hizo kukatwa kwa wakulima hao.

Alisema walikatwa kwa ajili ya bima ya mazao na nihuduma ambayo waliihitaji ili kutokupata hasara ya tumbaku pale inapotokea changamoto wakati wa kuhifadhi gharani au sokoni.

Hata hivyo aliiomba uongozi wa chama hicho kumwandikia barua ya kuomba fedha hizo zirejeshwe pamoja na kuondolewa kwenye huduma ya mazao ili aweze kuiwasilisha makao makuu ya benki hiyo.

Alisema yeye siyo msemaji wa mwisho na kuahidi suala hilo litafanyiwa kazi kwa wakati na fedha zao zitapatikana.

# Wenye ulemavu walia mazingira mabovu upigaji kura

**Na Waandishi Wetu.**

WATU wenye ulemavu wameomba Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kuandaa mazingira mazuri kwa ajili yao wakati wa kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu mwakani, tofauti na hali waliyokutana nayo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Ombi hilo limetolewa na Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Halmashauri ya Tarime Mjini, Mekaus Maingi.

Alisema kuna haja ya watu wenye ulemavu mazingira yao ya kupigia kura yaandaliwe vizuri ikiwemo vituo vya kupigia kura badala ya kuweka kwenye majengo ya miundombinu ya zamani.

Maingi alisema kero walizokutana nazo wakati wa kupiga kura ni pamoja na miundombinu, uongozaji wa watu wenye ulemavu hivyo kuwafanya baadhi yao kushindwa kutekeleza haki yao ya kikatiba.

Mengine ni pamoja na vituo kuchelewa kufunguliwa tofauti na muda uliopangwa na ubandikaji wa majina ya wapiga kura katika mbao za matangazo hayakuwa rafiki.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Shinyanga (SHIVYAWATA), Rehema Joshua alisema katika eneo lao walihakikisha watu wake wenye ulemavu wamepiga kura katika vituo vyote.

Alisema licha ya tatizo la miundombinu walikuwa wanapewa kipaumbe walipokuwa wakifika kwenye vituo pamoja na wazee wa miaka 60.

Alisema utaratibu huo ukifanyika katika uchaguzi ujao wenye ulemavu watapata fursa ya kuchagua viongozi wanaowahitaji.

**Imeandaliwa na Timothy Itembe (Tarime), Shaban Njia (Kahama).**

# Wanne mbaroni tuhuma wizi mbolea ya ruzuku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za wizi wa mbolea ya rukuzu mifuko 600 katika Wilaya ya Sikonge yenye thamani ya Sh.milioni 88.98.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora, Richard Abwao alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 24 mwaka huu majira ya saa 10:00 jioni.

Alisema meneja wa kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya Mkwawa Leaf Tobacco wilayani hapa aligundua kuibiwa kwa mifuko hiyo 600 sawa na tani 30.

Alitaja gari iliyobeba mbolea hiyo kuwa ni aina ya FAW yenye namba za usajili T.703 EDD na tela lenye usajili wa T.647 EDK likiwa na mbolea inayotajwa kuuzwa kwa mmoja wa wafanyabiashara mkoani Katavi aliyetambulika kwa jina la Crosi Singangala.

Kamanda Abwao aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Paulo James Milia (49) Athumani Kilatu na Eneza Nyika Eneza (37)

Alisema watuhumiwa hao akiwamo dereva wa gari hilo Tito Haule (48) walikamatwa baada ya upelelezi wa kina kufanyika, huku mfanyabiashara aliyenunua mbolea hiyo anaendelea kutafutwa baada ya kukimbia.

Kamanda Abwao alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paulo Chacha alisema serikali mkoani hapa kwa kushirikiana na vyombo vya dola na raia wema itakabiliana kwa nguvu zote dhidi ya watu watakaobainika kuihujumu sekta ya kilimo.

Chacha alisema kwamba dereva aliyekuwa akiisafirisha mbolea hiyo kutoka mkoani Songwe kuja wilayani Sikonge mkoani Tabora aliishusha mbolea hiyo akishirikiana na watu wengine na kuiuza kwa mfanyabiashara huyo baada ya kufika mkoani Katavi na kisha gari hilo kulitelekeza wilayani Sikonge.








# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 29, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


# Wanaharakati sheria, wacharuka na marekebisho haki ya mama msibani

**Na Elizabeth Zaya**



Waziri wa Katiba na Sheria Prof.Palamagamba Kabudi akiteta jambo na viongozi wa asasi MKUKI baada ya kuzindua kampeni ya siku 16 za Uanaharakati wa kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

KATIKA Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati wa kupinga ukatili huo wa kijinsia ikiwa ni kuelekea miaka 30+ ya Beijing mwaka kesho, Mtandao wa Kupinga Ukatili Tanzania (MKUKI), umebainisha mambo mengi yanayopaswa kufanyiwa kazi kukomesha vitendo hivyo, ikiwamo sheria za ardhi.

MKUKI wanasema, miongoni mwa yanayopaswa kushughulikiwa ni yanayogusa moja kwa moja familia, zikiwamo Sheria ya Ardhi ya Kimila na Sheria ya Ndoa, inayotumika sana kurudisha maendeleo ya kiuchumi kwa mwanamke, ikimnyima kumiliki mali kama alivyo mwanaume kwenye familia.

Inataja hata mke anapochangia kwenye ndoa yake kupatikana ardhi au mali nyinginezo na bahati mbaya mwenza wake akitangulia mbele za haki, mwanamke amekuwa akinyang`anywa ardhi.

Wanaitaja ni pamoja na mali nyinginezo alizoshiriki kuzipata, hivyo kuanza maisha upya, akitaabika na watoto wake.

### MKUKI WALIKOIBUKIA

Watetezi sheria wa MKUKI, anapaza sauti akiiomba serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na wizara nyinginezo za kisketa, kuliangalia hilo na kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali.

Hapo kuna eneo la ardhi ya kimila na Sheria ya ndoa ili kumnusuru mwanamke na kadhia hiyo ya ukatili ambayo imekuwa ikimdidimiza na kumrudisha nyuma kiuchumi.

Mwenyekiti wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), Dk. Monica Muhoja, anatamka haja ya kuongeza kasi zaidi katika kumuinua mwanamke.

Hilo linashauriwa kuendana na kutungwa sheria maalum za kupinga ukatili wa kijinsia, ambao umekuwa tatizo kubwa katika maisha ya mwanamke, hasa zile zinazogusa familia moja kwa moja.

"Kwa mfano, sheria za mirathi na Sheria ya Ndoa, zinabagua sana wanawake na mabinti husani wajane. Hizi zinachangia wengi kurudi nyuma kiuchumi na kupata matatizo ya afya ya akili kwa sababu wanakuwa wanakandamizwa sana," anasema.

Dk. Monica anaendelea: "Kwa hiyo tuko pamoja na serikali kushirikiana kuhakikisha vitendo hivi vinakomeshwa."

Anasema, tayari wamebainisha maeneo wanayotamani yafanyiwe kazi na kwamba, wako tayari kukaa na serikali kushirikiana kuyachambua kwa pamoja na kuona namna mbavyo wanaweza kutatua hilo.

"Mwaka huu tumekuja na maombi mengine ambapo tunaomba serikali kuyashughulia ikiwamo kulifikisha jambo hili kwenye agenda za kiusalama kwa kuhakikisha kuwa masuala ya ukatili wa kijinsia, yanaingizwa rasmi katika mipango na mikakati ya kiusalama ya kitaifa.

"Maombi mengine, ni pamoja na kuomba kutungwa kwa sheria mahsusi ambayo italinda jamii hasa wanawake na watoto dhidi ya unyanyasaji na ukatili huo wa kijinsia," anasema.

### KUTOKA UBALOZINI

Balozi wa Umoja wa Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya nchini, Christine Grau, anasema ukatili wa kijinsia ni tatizo la dunia na limekuwa likiathiri zaidi wanawake na watoto hivyo ni lazima kila mmoja apambane kulitokomeza.

"Tunaweza kuchagua kuiwezesha jamii kuzuia hili na namna ya kuwalinda wanawake na wasichana dhidi ya unyanyasaji huo wa kijinsia, kuripoti kesi na kutoa huduma bora kwa waathirika ikiwa ni pamoja na wale waliotengwa zaidi na walio hatarini,"anasema Balozi Christine.

Balozi wa Ireland nchini, Nicola Brennan, anasema kukomesha ukatili wa kijinsia inawezekana endapo kila mmoja atakubali kushiriki katika mapambano hayo ikiwamo kukataa kuozesha wasichana katika umri mdogo kabla ya kutimiza miaka 18.

Mratibu Mkazi wa Umoa wa Mataifa Tanzania, Suzan Namondo, anasema: "Tunapokaribia kuadhimisha Miaka 30 ya Beijing, tuna nafasi ya kutafakari namna ya kukabiliana na changamoto hiyo inayoendelea ya ukatili wa kijinsia na kupanga mbinu za dhati za kulitokomeza."

Anna Kulaya, Mkurugenzi wa WiLDAF, anasema dhamira ya kampeni hiyo ni kushawishi na kuhamasisha jamii kuondoa mitazamo inayochochea unyanyasaji na ukandamizaji kijinsia, kukuza usawa, heshima na haki kwa wote.

"Leo ni siku muhimu sana kwetu sote tunapoanza safari ya kuelekea Siku 16 za Uanaharakati wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

"Hii ni fursa ya kipekee ya kushirikiana, kuhamasisha na kuchukua hatua za pamoja dhidi ya aina zote za ukatili wa kijinsia kwa ajili ya jamii yenye us-


Inaendelea Uk 12

UCHUMI

MAELEKEZO YA RAIS WACHAGUA ENEO LAO...

# Moro inavyojikita kuzalisha karafuu ngazi ya visiwani; viwanda, mashamba vikimea

## • Katibu Tawala; wakulima tunawanoa Zanzibar, viwanda vyaja

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MWANAMO Februari mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, ametamka kuwa Sekta ya Viwanda, pia Utalii na Madini, zimevunja rekodi kuingiza mapato makubwa zaidi tangu Tanzania ipate uhuru.

Pia, mwezi Agosti mwaka huu akazungumzia mapinduzi viwanda mkoani Morogoro, akitamka bayana kwamba serikali iko tayari kubadilisha sera na sheria za nchi, ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, lengo kujihakikishia uzalishaji chakula cha kutosha kwa mahitaji ya ndani na nje.

Katika ufafanuzi wake, Rais Dk. Samia akasema serikali itaendelea kuwapa wakulima ruzuku ya mbolea na inajipanga kuwapa ruzuku za mbegu, ili kupunguza changamoto za uzalishaji mazao, wakulima wafurahie matunda ya kazi zao.

Baada ya Rais kuingia madarakani Machi 2021, mabadiliko makubwa yameanza kuonekana kwenye uchumi, mauzo ya nje ya bidhaa nchini, yameongezeka na kuvuka Dola za Marekani bilioni saba (shilingi trilioni 18) kwa mwaka kwa mara ya kwanza.

Hiyo inatajwa kuvuka Dola za Marekani bilioni saba kwa miaka miwili mfululizo; mwaka 2022 na 2023.

**USHUHUDA WA MORO**

Katika kuliunga mkono hilo, mkoa wa Morogoro umejiwekea mipango ya kuwa na mazao ya kimkakati kukuza uchumi wa wakulima na nchi.

Hiyo inajumuisha kuwekeza ili kurejesha historia viwanda, wakianza na vya mazao ya viungo vya chakula vikubwa vitatu, vya kati 10 na vidogo 50 vinavyotarajiwa kukamilika mwaka 2028.

Katibu Tawala wa Mkoa Dk. Musa Ally Musa, anasema mazao hayo ya viungo yana nafasi kubwa kuleta tija katika uchumi wa mkoa.

Anataja kilimo chenye tija Morogoro, mikakati yake ipo katika hatua mbalimbali za kuhimiza mazao hayo tajwa, kwa mwaka 2022 hadi 2025.

Vilevile, Katibu Tawala, anasema mwaka 2026 hadi 2028 wanahihimiza uanzishwaji viwanda na sasa mkoa una kiwanda kimoja cha viungo vya chakula viwanda vingine vidogo vitatu.

Pia, Dk. Musa anasema kuna viwanda vingine vidogo 50 vinavyoundwa na vikundi vya wanawake na vijana, ambao pia ni wakulima na wazalishaji wadogo wa bidhaa za viungo.

Rai yake, wakati umefika wakulima wakajikita kuzalisha viungo vya chakula, ili kuendana na mahitaji ya tani zaidi ya 100 kila mwaka kwa soko la ndani na nje ya nchi. Mpaka sasa inapatikana tani 30, sawa na asilimia 30.

Katibu Tawala anasema, mbali na karafuu, katika mazao viungo mengine ni; mchaichai, mdalasini, hiriki, karafuu, tangawizi, binzari, vanila, pilipili manga, vitunguu saumu na kakao yanayolimwa mkoani Morogoro.

Anasema ina masoko makubwa ndani na nje ya nchi, Morogoro inatoa tani 2000 za karafuu, sawaa na nusu zinazozalishwa Zanzibar kwa mwaka, ikikisiwa baada ya miaka mitano ijayo, Morogoro itaivuka tani 4000 za Zanzibar.

**UMAARUFU WA KARAFUU**

Kwa mujibu wa Dk. Musa, masoko yako dunia nzima yakiwamo nchini Uingereza, Canada na Ujerumani, anaitaja karafuu ina wateja wengiwanaitumia kwenye viungo vya chakula, dawa za meno, sabuni na hata sigara.

Dk. Musa anasema mkarafuu ukipandwa unahifadhi misitu na hauathiri mazingira, hivyo anawataka wakulima kuondoa hofu ya kilmo cha muda mrefu na kipato cha kila siku, kwa sababu inaweza kulimwa na mazao mengine ya muda mfupi katika eneo moja.

**UWEKEZAJI ULIVYO**

Uwekezaji kimkoa, Dk. Musa anasema serikali imeshajenga maghala matatu wilayani Morogoro, kuwasaidia wakulima kuhifadhi mazao yao, sambamba na kuuza na kupata malipo kupitia taasisi za kifedha, wakiondokana wizi, pia upokeaji pesa bandia.

"Suala la kulipwa fedha kupitia benki, linamsaidia mkulima kupata pesa nyingi, tofauti na kuuza kupitia rejareja inayomfanya mkulima kushawishika na kujiingiza kwenye mikopo," anasema na kuendelea:

Anafafanua, tayari mkoa umeshaunda Ushirika wa Kilimo cha Karafuu kwa kata nane za wilaya ya Morogoro, ili kuwawezesha kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha, zikiwamo benki kadhaa, waendeleze kilimo kwa manufaa yao na taifa

Anasema, bei ya karafuu ya Morogoro, katika soko la Dar es Salaam, inauzwa shilingi 28,000 kwa kilo moja dukani na mkoani Morogoro ni shilingi 23,000, akitetea sokoni hapo karafuu ni mali.

Dk. Musa anatumia mfano, wastani wa karafuu ingeuzwa shilingi 20,000 kwa kilo, wakulima wangeingiza shilingi bilioni 40 kwa mkoa na halmashauri husika zingepata shilingi bilioni 1.8 kwa zao karafuu.

Hapo anafafanua, kila ekari inachukua mimea ya karafuu 40 hadi 45 na inakisiwa ikizaa vizuri mkulima hakosi shilingi milioni kati ya tisa na 13 kwa mwaka.

"Familia moja yenye watu wanne hadi sita ina uwezo wa kupata (shilingi) milioni tisa hadi 3 kwa mwaka na hapo mkulima ana uwezo wa kutumia shilingi milioni moja kwa mwezi au laki nane kwa mwezi. Sasa kilimo hicho si ni sawa na mshahara wa mtu mwenye digirii?!" Anatoa tathmini Katibu Tawala huyo.

**CHANGAMOTO INAVYOKABILIWA**

Dk. Musa anasema, Morogoro kupitia mauzo ghalani, inajipanga kukabiliana na changamoto za wakulima hao wa viungo.

Anataja makonyo ambayo yangeweza kumuingiza fedha, lakini wachuuzi 'huwalalia' wakulima wakinunua klwa bei ya shilingi 500 badala ya 1,500 kwa kilo, kama ilivyo kwa wenzao wa Zanzibar.



Katibu Tawala wa Mkoa Dk. Musa Ally Musa, **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

Anasema kuwapo elimu ndogo ya karafuu, mkoa umeshawapeleka Zanzibar wakulima zaidi ya 50 kujifunza namna ya kuandaa shamba lake, hadi mavuno.

Katibu Tawala anafafanua kuwapo mapungufi ya usimamizi wa mashamba ya mikatafuu umewafanya baadhi ya wakulima kushindwa kuvuna inavyotakiwa.

Aidha, anasema wamejipanga kukabiliana na kushuka uzalishaji, wakitenga kundi la vijana wanaopatiwa vifaa na miche wapande kwenye vitalu na kuwauzia wataalamu kilimo kwenye ofisi ya mkoa na halmashauri kwa bei shilingi 1000 kila mche.

Dk. Musa anasema tangu mwaka 2022 kampeni ya kilimo cha mkarafuu ilipoanza, tayari miche 500,000 imeshagaiwa bure kwa wakulima na mkoa unatarajia kugawa miche milioni moja hadi kufika mwishoni wa mwaka huu.

Anataja baadhi ya maeneo ya mkoa yanakolimwa mazao hayo ni wilaya za: Morogoro, Gairo kwenye milima ya Nongwe, Mvomero - Turiani na Kilosa.

Dk. Musa anaiomba Wizara ya Kilimo kuwekeza kwenye mazao ya viungo na kusaidia utafiti na pembejeo, ili kufanya mazao hayo yawe rafiki kwa mazingira yao na kuleta tija shamabani.

Hata hivyo, annakiri Wizara ya Kilimo imejitahidi kuingalia sekta ya kilimo katika nyanja zingine.

**MAKATIBU TAWALA MSAIDIZI**

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mali Dk. Rosalia Rwegasira, anasema Morogoro ina malengo ya kuzalisha miche milioni mbili ya karafuu na kakao milioni 2.5, itakayosaimbazwa kwa wananchi.

Naye Katibu Tawala Msadizi (Viwanda, Biashara na Uwekezaji), Beatrice Njawa, anawataja mahsusi wanawake na vijana, kwa sasa wamejikita kuzalishaji mazao hayo ya viungo vya chakula, ingawa kuna changamoto ya kukosa nembo ya kudhibiti ubora (TBS).

Njawa anasema kuanzishwa viwanda Morogoro, kutawasaidia wakulima na wazalishaji bidhaa hizo, wakipata nembo za kufanya biashara ndani na nje ya nchi kwa maslahi yao na nchi.

**KUTOKA KIWANDANI**

Meneja uzalishaji wa kampuni inayojishughulika na kukausha mazao ya viungo Abel Gaima, anawataka wakulima kuongeza nguvu katika kilimo, kwani bado wanapata theluthi ya malighafu kutoka kwa wakulima, yaani tani 30, huku kunaa hitaji la tani 100 kwa mwaka.

Pia, anasema bei za bidhaa ya karafuu ni kubwa, tofauti na bidhaa nyingine, akitoa mfano kilo moja ni shilingi 19,500 kwa kilo.

Ofisa Usalama wa Chakula anayehusika na ukausha hiriki, Heavenlight Riziki, anaishukuru serikali mkoani kuhimiza jamii kujikita kwenye kilimo cha mazao viungo, akiamini inasaidia upatikanaji bidhaa hizo adimu, licha ya uhitaji mkubwa.

Hapo anaungwa mkono na mtumishi wa kampuni hiyo, mkuloim wa karafuu kutoka Kata ya Kibogwa Tarafa ya Matombo, Morogoro, Omari Saidi, anayeiomba serikali kuimarisha maghala ya wazi ya karafuu, kwa ufanisi wa tija ya uzalishaji na manufaa ya malipo yao.

Pia, anaiomba serikali ikaboresha miundombinu ya barabara na madaraja, kuwaepushia wakulima changamoto za uusafirishaji bidhaa zao, kutoka shambani hadi sokoni, pia kunufaisha wanunuzi wa bidhaa zao.

Pia, wakulima wanaiambia Nipashe, wanakabiliwa na ukosefu wa mashine ya kukatishia ushuru, hali inayofanya mapato ya mazao yao kutoingia kwenye baadhi ya Kata kama Matombo na kwenda kata jirani ya Kinole.

Taarifa ya Kilimo Mkoa, Morogoro ina eneo la hekta 2,226,396 linalofaa kwa Kilimo, lakii linalolimwa sasa ni wastani wa hekta 960,034 sawa na asilimia 43.

Pia, eneo linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji ni hekta 1,510,339.51 na eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni wastani wa hekta 79,429 sawa na asilimia 5 ambapo Mkoa una Skimu za Umwagiliaji 106 (asili na zilizoendelezwa) zinazotambulika zenye ukubwa wa hekta 323,758.15.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akasema licha ya biashara ndogo na za kati nchini kutoa ajira nyingi, inavochangia pato la taifa, kundi hilo la wazalishaji linakabiliwa na changamoto kama za masoko na kukosa mikopo.

Anasema, hivi sasa serikali iko mbioni kupitia Sera ya Uanzishwa Viwanda, Sera ya Taifa, Uwekezaji ya Mwaka 1996; Sera ya Maendeleo ya Viwanda (1996-. 2020) na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003), ili ziendane na mazingira ya sasa, kukidhi mahitaji.

# Wanaharakati sheria, wacharuka na marekebisho haki ya mama msibani

Inatoka Uk 11

awa, heshima na haki na maendeleo kwa wote.

"Muungano huu ulipoanzishwa ulikuwa na mashirika tisa tu, lakini kwa miaka kadhaa umeendelea kukua na kuvutia wanachama wengi, kutokana na juhudi zake za pamoja za kupinga ukatili wa kijinsia na kukuza usawa wa kijinsia katika jamii, lengo kubwa ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki katika nchi iliyo huru," anasema Kulaya.

Kulaya anaendelea; "Mkuki ni muungano mkubwa wa mashirika zaidi ya 200, unaofanya kazi chini ya uratibu wa WiLDAF ambayo dhamira yake kuu ni kushawishi na kuhamasisha jamii kuondoa mitazamo inayochochea unyanyasaji na ukandamizaji wa kijinsia, huku ikikuza usawa, heshima na haki kwa wote.

"Kupitia kampeni hii, MKUKI inalenga kuwa sauti ya mabadiliko na chachu ya jamii yenye amani, heshima, na utu kwa kila mtu bila kujali jinsia,"anasema.

**WAZIRI SHERIA**

Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi amesema serikali ipo tayari kuyapokea maombi hayo na kukaa kwa pamoja na wadau hao kuyajadili ili kuona namna gani hatua mbalimbali zinaweza kuchukuliwa.

Anasema suala la ukatili wa kijinsia ni la aibu linalobeza kundi kubwa katika jamii na si la kifahari kulitetea na kwamba linalohitaji kutokomezwa kwa kuchukua hatua stahiki.

Prof. Kabudi anasema licha ya Tanzania kupiga hatua katika mapambano katika eneo hilo, bado nguvu kubwa inahitajika kupiga hatua zaidi na kutaka kila mmoja awe balozi wa kupinga ukatili huo wa kijinsia.

"Kama ambavyo kaulimbiu ya kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wakijinsia inayosema Kuelekea 'Miaka 30+ ya Beijing', chagua kutokomeza ukatili' hii iwakumbushe watu wote kujitafakari na kujitathimini yale yanayofanywa kama yanatija," anasema Prof.Kabudi.

"Jambo hili halipaswi kuvumiliwa kabisa, hivyo niombe kila mmoja wetu tuendeleze mapambano ni ukatili, kazi hii iwe endelevu, isiishie kwenye hizi iku 16 na sisi kama serikali tutaendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia na kulinda utu wa mwanamke katika maeneo yote."

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hakika kwa SGR hii acheni iitwe SGR






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008 barua pepe:kulangwasos@gmail.com

JUZI kati hapa nikawa nimepata mwaliko wa harusi Dodoma, sikuwa na kisingizio cha kutokwenda, kwa sababu mwalikaji mwenyewe alishanikatia tiketi ya treni ya mwendokasi-SGR.

Shauku ya kutaka kupanda treni hiyo kwa mara ya kwanza, ikaongeza

kasi ya kukubali kwangu mwaliko bila kusita na moyoni nikajipangia kuwa na akiba yangu kwa lolote, huwezijua nini kinaweza kutokea baadaye.

Tiketi yangu nikatumiwa kwenye simu, ikinionesha siku ya kuondoka na muda, ambao ni saa 12 asubuhi, nikitakiwa kufika stesheni ya Dar es Salaam saa 10 alfajiri. Nani akatae? Nikawahi kulala ili niwahi kudamka.

Nililala mang'amung'amu, unajua tena siku ya kwanza kupanda dude ambalo unalisikia tu sifa zake kwa watu waliolipanda na wengine wakiongeza chumvi, hivyo nikataka nami hiyo chumvi nikaionje kama inatosha au imezidi.

Siku ya siku alfajiri, huyoo na bajaji mpaka stesheni na kuwahi kuingia huku nikilakiwa na wafanyakazi nadhifu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), wakinieleKeza kukaguliwa begi na vyote nilivyokuwa navyo, ikiwa ni pamoja na kuvaa mkanda na kisha kupanda juu ghorofa ya pili.

Eti ni kama kwenye ndege, ambayo sijawahi kupanda pia! Huko nako wengine wakinitaka nionyeshe tiketi, nikawaambia labda nikaichape kwa sababu iko kwenye simu! Ushamba bhana! Wakatabasamu tu na kuniambia ni hiyo hiyo ya kwenye simu. Kwa mshangao nikawapa, wakaitazamisha mahali kwenye kijiguzo hivi, nikaruhusiwa kuingia.

Nikidhani pengine ni wa kwanza kwanza kufika, aah wapi! Kumbe wenye shauku tuko wengi, kuna waliodamka kabla yangu wako kibao na viti ni vya kutafuta, kukaa kusubiri muda wa kuondoka. Nikapata kiti nikakaa huku shauku ikizidi kunilemea. Mgeni siku ya kwanza si mchezo.

Tukiwa hapo, mara tunatangaziwa kwenda kupanda, nababaika kidogo

kujua behewa langu, lakini naulizia na natazamiwa kwenye simu yangu na kuambiwa ni namba fulani na kiti fulani.

Hapo moyo unatulia, najifanya mwenyeji nakwea pipa la ardhini, najituliza kama si mshamba mimi.

Saa 12 asubuhi juu ya alama, nasikia honi na polepole 'gogo' linaanza kuondoka na kuchanganya kinoma.

Ghafla anakuja binti akisukuma kijitoroli mithili ya kijikontena fulani hivi chenye maji ya chupa, soda na majagi ya chai na kahawa.

Anaanza kuniuliza mimi niliyekaa dirishani, namwomba anipe chai na korosho (zingatia naomba). Ananipa karatasi laini yenye vipakiti viwili kama sigara hivi, kumbe ni sukari, ananipa bilauri ya plastiki yenye majimoto na kijifuko chenye uzi, kumbe ni majani ya chai kisha kijipatiki cha korosho.

Najikorogea pale na kuchana kijipakiti cha korosho. Ghafla ananiomba fedha! Hapo sasa, tuliozoea mabasi ya peremende na maji bure, naona kama naumbuka hivi, sikudhani nalipia. Nashituka kimoyomoyo najikaza kuulizia bei, ananiambia "elfu nne tu baba".

Naangalia ile bidhaa ya 'elfu nne tu baba', nguvu inaniishia, lakini nashika mfukoni kivivu na kutoa noti ya Sh 5,000 nampa, ananirudishia buku nalisondeka mfukoni huku sasa chai iliyowekwa sukari kama inageuka kuwa na shubiri.

Najipa nguvu, "potelea pwete," najisemea huku nikiangalia jinsi gogo lile linavyochanja mbuga sijapata kuona, najisahaulisha buku nne zangu.

He mara tunatangaziwa kufika Morogoro! Natazama saa, ni saa moja kama na dakika arobaini hivi, nashangaa.

Mahali ambako tulikuwa tukitumia saa nne mpaka tano, leo tunatumia saa moja na nusu na ushei kufika Morogoro?

Ukakasi wa chai unanitoka kabisa, najihisi kupata jambo la kusimulia siku nikirejea nyumbani. Dakika tano si nyingi, nasikia honi tena, hilo dude linatambaa kuitafuta Dodoma. Najifanya nimeshiba chai ile ya mang'amung'amu na kujipa matumaini ya kuvamia supu nifikapo Dodoma, kwa sababu harusi yenyewe ni jioni.

Kutokana na kudamka asubuhi, nikajikuta napitiwa na usingizi wa pono.

Naota mauzauza mengi tu, yakiwamo ya ghorofa la Kariakoo kuporomokea ndugu zetu, kuwaua na wengine kuwajeruhi.

Ghafla nashitushwa na abiria jirani yangu ambaye tangu tuanze safari hatukuwa tumebadilishana hata chafya, ananiambia: "Ndugu yangu tumefika, amka." Kweli nazinduka, naangalia saa ni saa nne kasorobo hivi. Nashangaa tena!

Mahali ambako awali tulitumia saa 10 kufika kwa basi, leo tunatumia saa nne tu, kweli? Hakika hii SGR iacheni iitwe SGR! Mbona ni mkombozi wa ajabu kwetu abiria tunaofanya safari za Dar-Moro na Dar-Dodoma na kurudi?

Kilichonishangaza zaidi, ni kumwona jamaa yangu fulani anayefanya kazi Mamlaka ya Usafiri wa Anga naye akiwa nasi na namsikia akisifia na kujiapiza kuwa ndege zitamsikia tu kwa SGR hii.

Tukashuka nikapanda bajaji hadi Area C kwa jamaa yangu, akanipokea na hakika jioni harusi ilikuwa nzuri.

Baada ya siku mbili, nikarudi Dar es Salaam, safari hii kwa basi! Ya humo we acha tu, nitakusimulia tukionana. Wenye mabasi hamtaniona tena kwenye mabasi yenu hakika. Si kwa mateso niliyopata! Mpao waitu!

UCHUMI

WALIOTELEKEZWA KILWA WAKOMBOLEWA ...

# Vijana wapewa mtaji, stadi uchumi katika jozi moja na elimu maalum

## •Operesheni yaanzia kata 10 za mfano

**Na Beatrice Philemon**

INAPOZUNGUMZIWA hali ya maisha ya vijana wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi kunatajwa wengi hawajihusishi na njia mbadala ya kujikwamua kiuchumi.

Inapotajwa wilaya ya Kilwa inahusisha maeneo kama: Kilwa Kivinje, Kilwa Masoko, Kijiji cha Njinjo na kata nyinginezo, wanategemea shughuli za uvuvi, pasipo kuwekeza katika shughuli nyinginezo za kiuchumi.

Dai kubwa ni kwamba, wamekosa watu wa kuwawezesha kujikita kiuchumi, wakiishia kuwa vijana wa hali ya chini.

Katibu Mtendaji wa taasisi isiyo ya Kiserikali ya Dira Yetu Initiative, Makame Juma, anaiambia Nipashe hilo katika uzinduzi wa mkakati wa miaka mitatu ya asasi hiyo kwa vijana, watoto na wanawake.

Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), baada ya kugundua changamoto, sasa unalenga kuwapa vijana stadi za maisha na uwezeshaji vijana kiuchumi, wajikwamue kiuchumi.

**KWANINI VIJANA?**

Anasema, wameamua kuja na mkakati huo, baada ya kugundua vijana wengi wa Kilwa wako katika umasikini na wengi wametelekezwa na wazazi, watoto wanajilea wenyewe.

Makame anasema, kuna kundi la vijana waliojikita katika biashara ndogo, ambazo haziwezi kubadilisha maisha yao na kuna asilimia walioko katika shughuli za uvuvi, kwa sababu wengi hawakusoma na maisha yao ni magumu.

"Wakati wa utekelezaji wa mkakati huu, vijana ambao wapo shuleni na vijana ambao hawapo shuleni, yaani wale ambao wameshindwa kuendelea na elimu ya msingi na sekondari kutokana na changamoto mbalimbali za kifamilia, watafundishwa kilimo hai ambacho ni rahisi na rafiki wa mazingira," anaeleza.

Makame anataja, pia watafundishwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wakitengeneza viatilifu vya asili vinavyodhibiti wadudu waharibifu wa mazao shambani, kwa kutumia mimea ya asili

Imani yake Makame anaitaja, itawasaidia kujikwamua kiuchumi, kupunguza wimbi la vijana wasio na ajira wilayani Kilwa, w wanapat ajira, maarifa na ujuzi mbalimbali, hata wakajikita katika sekta nyinginezo, badala ya kutegemea uvuvi pekee.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Njinjo ni sehemu ya wanufaika wa mradi huo wilayani Kilwa, mkoani Lindi. **PICHA: MTANDAO**

Hadi sasa inatajwa kuna wanachama wawili kutoka Taasisi ya Dira Yetu Initiative wamepata mafunzo ya kilimo hai katika Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) kwa muda wa siku tano.

Hapo ina maana ya kuwafundisha vijana wa Kilwa waweze kujitegemea na kuinua kipato chao. Makame anaendelea:

"Lengo letu ni kuona jamii ya KIlwa isiyo na umasikini, stahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi na yenye maendeleo na ustawi endelevu ikizingatia usawa wa haki za watoto."

Makame anaeleza: "Wakati wa kutoa mafunzo, tutashirikiana na watu waliopata mafunzo kuhusu kilimo hai, maofisa kilimo na walimu wa klabu za wanafunzi kutoka shule mbalimbali za msingi na vijana ambao hawapo kwenye mfumo rasmi tutawapata kupitia mikutano ya vijiji au 'public announcement' (tanagzo la umma)."




Hapo anataja dira ya asasi hao inayojihusisha na kupinga ukatili dhidi ya watoto, kukuza stadi za maisha na uwezeshaji wa vijana kiuchumi, inalenga "kuchochea upatikanaji wa huduma bora za elimu jumuishi shuleni na mabadiliko ya tabia nchi."

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Asasi ya Dira Yetu Initiative, imefika katika vijiji 10 vilivyopo kata za Kilwa Singino, Mandawa, Lihimalyao na Njinjo kupitia makundi ya wanawake, vijana na watoto.

**SHUGHULI KIJAMII**

Inatajwa makundi ya kijamii ambayo yameshanufaika kwa mfano hayo yanajumuisha, walimu na watoto kupitia vilabu vya shuleni, Makame akisema wakinolewa katika maeneo ya; mabadiliko ya tabianchi, elimu ya upandaji na utunzaji miti, pia umuhimu wa usafi mazingira shuleni.

Kwingine kunakotajwa ni upandaji mikoko katika pwani ya Kilwa Masoko na Kilwa Kivinje, jumla ya mikoko 35,000 ilipandwa, kwa kushirikiana na sasi nyinginezo, pia wamefanikiwa kusambaza miche 940 ya miti ya vivuli, matunda na mbao kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Ni manufaa yanayoziangukia shule 10, zikiwamo zilizopewa miche; Nangulukuru, Mandawa, Lihimalyao Kaskazini, Mikindani Centre, Kisongo, Mzizima, Kipindimbi na Shule ya Sekondari Njinjo.

**KWANINI MICHE**

"Tulitoa miche hii ili kuunga mkono serikali na wadau wengine na mashirika binafsi katika harakati za kupambana na mabadiliko ya tabianchi, wanafunzi kupata kivuli, kuzuia upepo mkali shuleni, kusaidia wanafunzi kupata matunda, ili kuboresha afya zao, pia kujiongezea kipato kwa kuuza matunda na mbao," anasema

Makame anasema kuna la kujivunia kuwapo matokeo chanya ya usambazaji miche hiyo shuleni,ikistawi kwa ufanisi ikiwamo miti ya mitiki na mapera.

**ELIMU YA MABADILIKO**

Kukiwapo vilabu 10 vya wanafunzi katika shule za msingi 10, kila moja ikiwa na wanachama 25, waloandaliwa wakawafunze wenzao, wakiwa mabalozi katika jamii zao.

Kwa mujibu wa Makame, maudhui ya madarasa hayo ya mazingira yanajumuisha madhara ya: Ukataji miti ovyo, utupaji taka, pia kukata miti katika vyanzo vya maji.

Mengine ni athari za: Kilimo cha kuhama, kuwa na mifugo mingi katika eneo moja, akitaja ni hali inayojitokeza hata wilayani Kilwa iliyovamiwa na kundi la wafugaji kutoka mikoa ya Kaskazini na Kati.

Vilevile anatamka wanafundisha watoto hasara za ukataji miti ovyo kunavyosababisha mmomonyoko wa ardhi, upungufu wa mvua na kukauka vyanzo vya maji.

"Tumeamua kutoa elimu hii kwa sababu watu wanatupa taka kwenye vyanzo vya maji na pia miti inakatwa kwenye vyanzo vya maji ambapo imesababisha chanzo cha maji cha Mlima Kitumba kilichopo kata ya Kivinje Singino kukauka," anasema Makame.

**MWANAIDI BILALI**

Mwanaidi Bilali, Mwenyekiti wa Asasi ya Dira Yetu Initiative anasema mbali na hilo, vijana watafundishwa namna ya kuandaa matuta ya kina kirefu wakitandaza matuta, namna ya kuotesha mbegu na kutumia mbolea za kupandia.

Anasema, pia watafundishwa kutengeneza samadi kwa njia ya asili kupandia mazao, huku wakitengeneza viuatilifu vya asili kwa ajili ya kudhibiti na kuua wadudu waharibifu

Pia asasi itaendelea kutoa elimu kwa vijana namna ya kutumia fursa zinazowazunguka au zilizopo katika maeneo yao ili kujikwamua kiuchumi.

Hadi sasa, anasema fursa zilizopo kwa vijana katika wilaya ya Kilwa ni ardhi na uchumi wa bluU, vijana wana uwezo wa kufanya shughuli za kilimo kama kilimo cha mboga na matunda, ufuta hata mahindi kwa kutumia rasilimali ardhi iliyopo katika maeneo yao ya vijiji.

Pia, anaahidi wataendelea kuhamasisha vijana kujiunga na vyuo vya ufundi na ujuzi ili kujiendeleza kimasomo, kuongeza ujuzi na hatimaye waweze kuzalisha bidhaa au mazao yenye ubora.

Lingine ni kwenda kwenye vikundi vya vijana na wanawake kutoa elimu ya kilimo hai, kwa kuanza na vikundi vya vijana na wanawake katika kata ya Mandawa, Matandu na Miguruwe na baadae watakwenda katika Kata nyingine.

"Kilimo hai, hakiitaji pesa, kinahitaji rasilimali za miti au mimea au viuatilifu kutoka kwenye mimea," anasema.

Anajisifu watoto kuanza kujua jinsi ya kutunza miche ya miti inayopelekwa shuleni, huku wameshawapatia plasiki za kuhifadhi maji safi na salama ya kunywa na kunawa mikono, wakitoa elimu kwa watoto juu ya haki na wajibu wao katika utoaji wa huduma bora za elimu na miundombinu ya usafi shuleni.

Jumla ya mikutano 10 ya kujengea uwezo watoto kuhusu usafi wa mazingira shuleni, kujua nafasi yao katika kushawishi serikali kuboresha miundo mbinu ya elimu imeshaifanyika katika shule za msingi 10.



# Katibu Tawala aanza 'vita' kutokomeza kipindupindu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk.Fatuma Mganga amewaagiza wataalamu wa afya kupima sampuli za maji katika maeneo tofauti mkoani hapa, ili kubaini visima vyenye vimelea vya ugonjwa wa kipindupindu.

Alitoa agizo hilo juzi katika kikao kazi cha timu ya uratibu wa afya mkoa kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu.

Dk.Mganga alisema suala la kupima maji ni la muhimu sana kwani yakibainika yana vimelea vya ugonjwa wa kipindupindu itakuwa rahisi kuyatibu na kuepusha matumizi yake kwa wananchi wa maeneo husika.

Alisema timu ya uratibu wa afya mkoa inatakiwa kuwajibika kwa kuhakikisha wanajituma na kufanya kazi kwa weledi ili kuepusha mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika Mkoa wa Singida.

"Katika kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu mnatakiwa kutibu maji yote yanayotumika vijijini na visima vya watu binafsi majumbani, kuhakikisha kila kaya ina choo cha kutumia," alisema.

**"Katika kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu mnatakiwa kutibu maji yote yanayotumika vijijini na visima vya watu binafsi majumbani, kuhakikisha kila kaya ina choo cha kutumia,"**

Aidha, alisema timu hiyo inatakiwa kuweka kambi yenye vifaa vya kutosha katika maeneo hatarishi na kuhakikisha shule zote za msingi na sekondari zina vyoo na sehemu za kunawa mikono.

"Kila mmoja wetu hapa ahakikishe anawajibika ipasavyo katika kuunga mkono juhudi za kupambana na kipindupindu,wadau wote kila mmoja atumie nafasi yake kwa matokeo mazuri ya mpangokazi na kuleta mrejesho wa utekelezaji wa majukumu yake," alisema.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Singida, Sebastian Mgeta, alibainisha visababishi mbalimbali vya ugonjwa wa kipindupindu kuwa ni pamoja na ukosefu wa maji safi na salama katika maeneo yenye mlipuko.

Alitaja sababu nyingine ni ukosefu wa vyoo katika kaya, baadhi ya kaya kutotumia dawa za kutibu maji, imani potofu na kuchelewa kwenda kupata matibabu pindi tu dalili zinapoonekana.



Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Joanfaith Kataraia (kushoto), akizungumza na wenyeviti wa mitaa, vijiji na wajumbe kabla ya kuapishwa, mjini Singida jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# RC akipongeza TIA kupandisha hadhi tawi la Singida

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imeipongeza Taasisi ya Uhasibu nchini (TIA) kwa kupandisha hadhi chuo hicho tawi la Singida kupitia maboresho ya miundombinu mbalimbali ikiweno majengo na taaluma sambamba na kutoa shahada ya uzamili.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema hayo kwenye mahafali ya 22 ya chuo hicho na ya 13 kwa tawi la Singida yaliyofanyika mkoani Singida juzi.

Dendego, alisema maboresho hayo makubwa yanadhihirisha ukubwa wa chuo ambacho sasa kimeongeza wigo na fursa kubwa kwa kundi la vijana kuweza kupata maarifa na ujuzi zaidi, utakaoendana na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi. "Serikali itaendelea kushirikiana na wanafunzi na uongozi wa chuo hiki...naomba sana mkitumie chuo hiki kujipatia maarifa mengi kwa ajili ya kuitumikia jamii yetu kupitia nyanja zote" alisema Dendego.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Palangyo alisema, kuanzishwa kwa shahada ya uzamili katika tawi la Singida ni hatua kubwa na muhimu ambayo itachochea maendeleo na ongezeko kubwa la wanafunzi, hasa wale wanaotarajia na kutamani kujiunga na chuo hicho.

"Mpaka sasa, tayari tumesajili wanafunzi 66 wa shahada mpya ya uzamili, iliyoanza kutolewa hapa chuoni kwetu...wanaendelea kupata maarifa na ujuzi zaidi kwa faida yao binafsi na taifa kwa ujumla," alisema Profesa Palangyo.

Naye mjumbe wa Bodi ya TIA, Renatus Msangira aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Bodi, alihimiza umuhimu wa wananchi kutumia vizuri fursa ya uwepo wa chuo hicho mkoani Singida kuweza kuongeza maarifa zaidi yatakayoboresha maisha yao.

Mahafali hayo yaliyohusisha wahitimu 1,477 kampasi ya Singida wakiwemo wanawake 812 sawa na asilimia 55 na wanaume 665, idadi hiyo ni sawa na asilimia 13 ya wahitimu wote 11,620 wa kampasi za Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Kigoma na wenyeji Singida. Wahitimu walitunukiwa vyeti kwa ngazi mbalimbali, ikiwemo cheti cha awali, cheti, stashahada na shahada, kwa fani za mahusiano ya umma, uhasibu, uongozi wa rasilimali watu, usimamizi wa biashara na ununuzi na ugavi.

# Watoto wenye uhitaji kupata elimu bila kikwazo

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Janeth Mayanja amesema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili watoto wenye uhitaji maalumu waweze kupata elimu bila kikwazo.

Mayanja, aliyasema hayo juzi wilayani Chamwino baada ya kukabidhiwa vifaa vya ujenzi wa jengo la jiko katika shule ya msingi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu Buigiri, vilivyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Alisema serikali itahakikisha inashirikiana na wadau mbalimbali wa elimu katika kuunga mkono kama ilivyofanya kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambayo imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jiko la kupikia chakula cha wanafunzi hao na walimu.

Alisema, kutokana na mchango huo serikali ya wilaya itahakikisha kuwa mchango huu uliotolewa utaenda kufanya kazi iliyokusudiwa na ujenzi utakamilika kwa wakati ukizingatia kuwa kila kitu kipo.

"Mimi kama Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na watendaji wangu nitahakikisha ujenzi wa jiko hili unakamilika ukizingatia kila kitu kipo na hata fedha ya kuwalipa mafundi ipo hivyo naomba likamilishwe haraka kama ilivyokusudiwa" alisisitiza.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa alisema kuwa katika kuadhimisha Siku ya Takwimu Afrika wameamua kutoa mchango wao wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa jiko la kupikia chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum Buigiri

Alisema mchango uliotolewa ni tofari 700, saruji mifuko 27, bati za rangi 25, mbao 24, misumari, rangi na fedha kwa ajili ya fundi Sh. 500,000 wote ukiwa na thamani ya Sh. milioni 3.9.

Alisema katika kuadhimisha Siku ya Takwimu Afrika wameamua kuungana na watoto hao lengo ni kuhamasisha matumizi ya takwimu katika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo.

Yohana John, mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo aliipongeza Ofisi ya Takwimu kwa kuona umuhimu wa kuwatembelea na kutoa mchango kwa ajili ya ujenzi wa jiko.

Alisema jiko hilo litawasaidia kuboresha mazingira ya uandaaji wa chakula kwa ajili ya matumizi yao na walimu tofauti na ilivyo kwa hivi sasa.





# Watendaji watwishwa zigo kuhimiza lishe bora kwa wajawazito, watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATENDAJI wa kata za Halmashauri ya Mji Njombe wametakiwa kuendelea kuhimiza lishe bora kwa wajawazito na watoto wachanga.

Pia wametakiwa kuhakikisha watoto wananyonyeshwa kwa kipindi cha siku 1,000 za mwanzo ili kupambana na udumavu.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa viashiria vya mkataba wa lishe kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024.

"Tumepiga hatua kubwa katika jitihada za kupunguza udumavu, nimeona kampeni zinafanyika na siku za afya na lishe tulizungumza hapa suala la kuwafuatilia wajawazito na kina mama wanaonyonyesha ni muhimu sana, lazima tuendelee nalo kwa bidii tusiache ili tubaki kuwa na alama ya kijani," alisema Kissa.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Njombe Dk. Jabil Juma alitoa msisitizo kwa watendaji kuendelea kufuatilia lishe za watoto shuleni kwa kuhakikisha kila shule wanafunzi wanapata chakula chenye virutubisho sambamba na kuhimiza uwepo wa bustani za mboga.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji Njombe, Fransisca Mosha aliwasisitiza watendaji hao kuwafuatilia wajawazito kwa karibu ili kupambana na changamoto ya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu ambao wamepungua kutoka asilimia 10.2 hadi asilimia 8.56.

"Niwaombe watendaji tusimame kidete na wajawazito tusiwaache ili kupambana na changamoto ya watoto kuzaliwa na uzito pungufu. Tumepiga hatua lakini bado," alisema Fransisca.

> **"Niwaombe watendaji tusimame kidete na wajawazito tusiwaache ili kupambana na changamoto ya watoto kuzaliwa na uzito pungufu. Tumepiga hatua lakini bado," alisema Fran-**

Alisema kitengo cha lishe kwa kushirikiana na wadau wa USAID Lishe Project, katika kipindi cha Julai -Septemba 2024 imefanikiwa kutoa elimu ya unyonyeshaji kwa wanawake 65 wenye watoto wenye umri chini ya miaka miwili, ikiwa ni jitihada za kuboresha afya ya mama na mtoto ili kupambana na udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5.

Alifafanua kuwa elimu hiyo ililenga kuwahamasisha na kuwaelimisha wanawake kuhusu umuhimu wa kunyonyesha watoto kwa kipindi chote cha siku 1000 lishe ya familia kwa ujumla.

Mdau wa lishe kutoka mradi wa USAID Lishe Project, Lilian Kipeta alitoa rai kwa watendaji kuendelea kutoa elimu sahihi ya lishe kwa kina mama pamoja na kuadhimisha siku ya afya na lishe kama mwongozo unavyotakiwa kwa kuhakikisha jamii na wataalamu wote katika kata wanashiriki kikamilifu.

"Njombe mnafanya vizuri, inatia moyo, jitihada hizi ziendelee na sisi tupo nanyi bega kwa bega na kikubwa tuhakikishe tunawafuatilia waliogundulika kuwa na changamoto ili wasiwe sababu yakuturudisha kwenye alama nyekundu," alisema Lilian.

Katika kikao hicho imeshauriwa wadau kuona umuhimu wa kuandaa warsha ya elimu ya lishe kwa wanaume lengo ikiwa ni kuhakikisha baba pia anashiriki kikamilifu katika juhudi za kuhakikisha lishe bora inapatikana kwa familia nzima.



Mkufunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe Ndaki ya Mbeya, Prof. Hawa Tundui akiongoza maandamano ya kitaaluma, wakati wa mahafali ya chuo hicho, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wazee, wajawazito waridhishwa mazingira kupiga kura

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAKUNDI maalumu wakiwemo wazee, wajawazito, kinamama wenye watoto wadogo mkoani Njombe wamesema wameridhishwa na mazingira ya kupiga kura kwa wakati na kurudi nyumbani.

Wakizungumza juzi baada ya kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Lunyanywi uliyopo Kata ya Mji Mwema Halmashauri ya Mji wa Njombe wamesema mazingira ya upigaji kura yameboreshwa kuliko kipindi cha nyuma.

Mmoja wa wananchi hao akiwemo, Mariam Mwalepelo alisema wamehamasika kuja kupiga kura kwa sababu ya mazingira rafiki kwa makundi maalumu.

"Nilivyofika katika kituo hiki msimamizi alinipa kipaumbele kwa sababu nimembeba mtoto ili kuweza kuendelea na majukumu mengine kwa hiyo nimepiga kura mapema nashukuru kwa hii nafasi," alisema Mariam.

Naye Amon Mbando alisema mazingira yameboreshwa ili kumfanya kila mtu apige kura kwa kuzingatia makundi maalumu na kwa siri bila ya kupata adha yeyote.

Mratibu wa Uchaguzi Mkoa wa Njombe, Christina Mzena alisema walijipanga katika kuhakikisha wanaboresha mazingira kwa makundi maalumu ili wapate fursa ya kupiga kura.

Msimamizi wa uchaguzi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Namsifu Maduhu alisema hakujatokea tatizo lolote tangu kipindi cha kampeni hadi wakati wa uchaguzi.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alisema kujitokeza kwa wananchi kupiga kura ni fursa kwao kuchagua viongozi wanaowataka kwa ajili ya maendeleo ya mitaa yao.

# REA kugawa mitungi 13,000 wilaya nne

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKALA wa Nishati ya Umeme Vijijini (REA) wanatarajia kugawa mitungi ya gesi zaidi ya 13,000 ya bei nafuu katika wilaya nne za Mkoa wa Njombe ili wananchi waondokane na matumizi ya mkaa.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Nishati Jadidifu na Teknolojia Mbadala, Advera Mwijage wakati akitoa taarifa kwa Katibu Tawala Mkoa wa Njombe ofisini kwake.

Alisema kila wilaya itapata mitungi 3,255 ambayo itauzwa kwa nusu bei ya kawaida na huku nusu iliyobaki italipiwa na serikali. "Katika mkoa huu tumepata mtoa huduma ambaye anaitwa Taifa Gesi na atasambaza mitungi 13, 020 katika wilaya nne za Mkoa wa Njombe na tunaamini mitungi hii itafika kila wilaya na utaratibu wa utoaji wa mitungi hii itauzwa kwa bei ya asilimia 50," alisema.

Alisema lengo la mpango huo ni kuwapunguzia adha wananchi kwa kuwa gharama za gesi zimekuwa kikwazo kwa kaya za kipato cha chini na kwamba vitambulisho vya taifa vitatumika katika ugawaji wa mitungi hiyo.

Hata hivyo, aliwataka wakazi wa mkoa wa huo kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika vituo vya mafuta vijijini utakaofanyika kwa fedha za mkopo ambapo wanufaika ni pamoja na wananchi, wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta na vikundi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Miundombinu wa Mkoa wa Njombe, Joseph Rutashibilwa alisema Njombe inakabiliwa na tatizo la matumizi ya kuni na mkaa ambayo yanaathiri mazingira na afya za wananchi, hivyo wanayo imani mpango huo utasaidia kupunguza athari hizo.

Baadhi ya wananchi, akiwemo Anna Mtitu alisema kutokana na gharama ya gesi kuwa juu inawalazimu kutumia mkaa licha ya kuwatelea madhara.

"Ni kweli mkaa unamadhara lakini kinachonishinda kutumia gesi pekee ni kutokana na kipato kwa sababu nikitumia mkaa kupikia chapati kifua kinaniuma sana," alisema Anna.

Naye Mina Mbwambo alisema matumizi ya gesi yanasaidia kufanya kazi kwa haraka na mkaa kwa mwezi unaweza ukatumia magunia hadi matatu kwa mwezi lakini gesi unatumia zaidi ya miezi miwili.



# Bosi polisi ataka wafungwa kupewa elimu ya kiroho

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amesema ni muhimu Jeshi la Polisi kushirikiana na viongozi wa dini katika kuwapatia elimu ya kiroho wafungwa na watuhumiwa waliopo gerezani ili kubadili maisha yao.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kabi, ambapo mazungumzo yao yalilenga kuimarisha ushirikiano kati ya Ofisi ya Mufti na Jeshi la Polisi kwa maslahi ya usalama wa wananchi na ustawi wa jamii.

Kamishna Hamad alisema elimu hiyo itasaidia wafungwa hao baada ya kumaliza kifungo gerezani kurudi katika jamii wakiwa na maadili mema.

Aidha, alisema katika kukuza amani na utulivu ni jukumu la viongozi wa dini katika kuhubiri amani na mshikamano wa taifa na kuwaelimisha waumini juu ya umuhimu wa kufuata sheria na kuheshimu mamlaka za kiserikali.

Alisema ni muhimu pia kuimarisha mshikamano kati ya madhehebu mbalimbali ili kupunguza migogoro ya kijamii na kupambana na uhalifu na tabia hatari zinazokinzana na dini.

Pia, aliwataka viongozi wa dini kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kufuata sheria za barabarani ikiwa ni pamoja na matumizi ya kofia ngumu, leseni na kuendesha vyombo vya moto, madereva kutotumia kilevi, kufundisha maadili bora kama vile kuheshimu mali za umma na kutopokea au kutoa rushwa.

**Alisema ni muhimu pia kuimarisha mshikamano kati ya madhehebu mbalimbali ili kupunguza migogoro ya kijamii na kupambana na uhalifu na tabia hatari zinazokinzana na dini.**

Hata hivyo, alisema ni vyema viongozi wa dini kuwaelimisha vijana kuhusu wajibu wao kwa jamii na umuhimu wa kuwa raia wema, kuimarisha malezi bora kwa vijana na dini inaweza kusaidia kuwarekebisha vijana wanaojiingiza katika tabia hatarishi.

Alisema walinzi wa nyumba za ibada wanahitaji mafunzo juu ya usalama na tahadhari za dharura, lakini pia jamii kukabiliana na changamoto za kijamii zinazohusiana na mila na desturi na jinsi ya kukabiliana na mila na desturi zinazokinzana na mafunzo ya dini, kama vile uchawi na imani potofu.

Mufti Mkuu, Shekhe Saleh Omar Kabi alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na kulitaka jeshi hilo kuongeza bidii katika kulinda maisha ya watu na mali zao.

Alisema jeshi hilo lina miundombinu mizuri ya kutunza amani ya nchi na kulipongeza kwa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi ambavyo vimesaidia jamii kuondokana na vitendo vya kihalifu.



Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad (kushoto), akizungumza na Sheikh Mkuu Zanzibar, Saleh Omar Kabi mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mitaala ya elimu yafumuliwa kuendana soko la ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya marekebisho ya mitaala kwa kuanzisha dhana ya mahiri katika kujifunza, ili kuwawezesha wanafunzi kuendana na mahitaji ya soko la ajira na uchumi wa kisasa.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Husein Abdulgulamu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe Ameir Abdallah Ameir.

Ameir alitaka kujua wizara inajiandaa vipi kutoka katika ufaulu wa matokeo (grade) kuelekea kwenye ufaulu wa uchumi na ajira.

Alisema upimaji wa upatikanaji wa elimu utakwenda sambamba na aina ya taaluma ambayo mwanfunzi anapewa kama vile ujuzi maalumu, teknolojia, ujasiriamali, na mafunzo ya vitendo ambavyo vinawasaidia wanafunzi kuwa na uwezo wa kushindana kwenye ajira pamoja na kujiajiri.

Alisema upimaji wa mwanafunzi kwa mfumo wa grade una faida mbalimbali zikiwemo kurahisisha uwekaji wa viwango vya ufaulu kwa wanafunzi, kurahisisha uelewa wa matokeo kwa wadau, kuongeza jitihada katika ufundishaji na kurahisisha upangaji wa wanafunzi katika viwango mbalimbali vya ufaulu.

Aidha, alisema upimaji wa mwanafunzi kwa mfumo wa grade una hasara mbalimbali zikiwemo kusababisha msongo wa mawazo na kuwajengea hofu walimu na wanafunzi iwapo watapata alama (grade) za chini.

Alisema Wizara ya Elimu inatarajia kujenga karakana katika vyuo vyote vya ufundi ili wanafunzi kusoma kwa vitendo na baada ya kumaliza masomo kujiajiri na kuajiriwa.

# Serikali: Zanzibar ina madaktari 749, bingwa 89

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa Zanzibar ina madaktari 749, kati ya hao 89 ni madaktari bingwa, 336 wenye kiwango cha elimu ya shahada na 324 ni maofisa tabibu wenye elimu ya kiwango cha stashahada.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh alisema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi Mwanakwerekwe Ameir Abdallah Ameir aliyetaka kujua kwa sasa Zanzibar ina madaktari wangapi wa kiume na wangapi wa kike kwa mujibu wa takwimu za serikali.

Akijibu swali hilo, Hassan alisema madaktari wanawake ni 410 na wanaume ni 339 ambapo tofauti hiyo ni ya kimatokeo.

Aidha, alisema kwa kuwa wanaosoma taaluma ya udaktari bado ni kidogo, wizara haijaweza kuweka mikakati maalum ya uajiri, bali wale wote wanaomba kazi huajiriwa na wala wizara haina mkakati wa wanaume na wanawake wangapi bali ni matokeo ya waliomba.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imesema kuwa imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali katika kudhibiti uchimbaji na usafirishaji haramu wa maliasili zisizorejesheka.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Zawadi Amour Nassor, alisema miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na wizara katika kulinda maliasili zisizorejesheka ni kufanya doria usiku na mchana hususani katika maeneo ambayo uchimbaji haramu umekithiri.

Alisema licha ya jitihada, wizara bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika kulinda maliasili zisizorejesheka.

Alizitaja changamoto hizo ni pamoja na kuvuja kwa taarifa za doria kupitia mtandao uliowekwa na wachimbaji pamoja na wasafirishaji wa maliasili zizisorejesheka kinyume na utaratibu.

"Changamoto zingine ni baadhi ya wananchi kuficha taarifa za wachimbaji haramu kwa makusudi au kwa kuhofia usalama wao, baadhi ya viongozi kusimama mstari wa mbele kuwatetea wahalifu kwa sababu za ujamaa au kisiasa," alisema.

Aidha alisema licha ya changamoto hizo wizara bado inaendelea kujiimarisha katika udhibiti wa uchimbaji haramu wa maliasili zisizorejesheka ikiwemo kukiongezea nguvu kikosi cha doria pamoja na kuanza taratibu za kutumia teknolojia katika udhibiti wa maliasili zisizorejesheka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



Jina : **SAFI OCTAVIAN MWINGILIHELA** Cheti Kilichopotea : Cheti cha Chuo NTA level 5 Chenye Index Namba **NS1488/0050/2012** (Technical Certificate in Pharmaceuticals) kilichotolewa na NACTE Mwaka 2021 Taarifa ya Polisi: Namba **PHQ/NJO/NJO/375/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



JINA: **NEEMA PAULA MATHEW.** Anatangaza kupotelewa na CHETI CHA **ADDO INDEX NO 0822114.** Taarifa ya Polisi: Namba **PHQ/DAR/ILA/260836/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKI PIKI

**FESTO ADRIANO MWITA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE CARD YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 559 DKJ,** AINA YA BOXER (150)-NYEUSI ,JINA LA KWENYE USAJILI WA KADI YA PIKIPIKI MOHAMMED ENTERPRISED LTD. KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/37090/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**SUBIRA JUMA NGALUMA** anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye namba za usajili, **T 127 ACB** Toyota Hiace, **T 141 AKQ** Toyata Hiace, **T 835 BLR** Nissan caravan na **T 529 CSH** Nissan caravan. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/TAN/12879/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**

**RUFAA/MADAI/NA 7973/2024**

**Shauri ya Rufaa Jinai/Madai Na 7973/2024**

**Katika Mahakama ya Wilaya ya DODOMA**

**ABASA ALLY MUSSA.................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**SOKONI MICROFINANCE LTD................MRUFANIWA**

**Kwa SOKONI MICROFINANCE LTD**

Kwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa tarehe 13 Mwezi 01 Mwaka 2025 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamojana vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 21 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 423 LA 2024**

**DONAT MICHAEL MOSHI.........................MUOMBAJI /WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **BORA SAMWEL MARWA**
2. **AUGUSTINE VUMA HOLLE MDAIWA/WADAIWA**
3. **KAPALAMA AUCTION MARK**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **BORA SAMWEL MARWA**
2. **AUGUSTINE VUMI HOLLE**
3. **KAPALAMA AUCTION MARK**

**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**DONAT MICHAEL MOSHI** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 15/01/2025 saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 Mwezi 11, 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 131 YA 2024**

**MWESIGWA ELTON FELICIAN MDAI/WADAI**

**DHIDI**

**MOHAMED JANMOHAMED MDAIWA/WADAIWA**

**KUITWA SHAURINI**
**MOHAMED JAN MOHAMED MANJI**

**Popote ulipo/Mlipo,**

**MWESIGWA E. FELICIAN** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Temeke. Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 11/12/2024. Hivyo basi unatakiwa /mnatakiwa kuleta utetezi wako/wenu ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba TEMEKE. Endepo hautatekeleza/hamtatekeleza haya Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 13/11/2024

MWENYEKITI,
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ILALA**

**Kituo cha KARIKOO Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Na. 396 /2024**

**Jina la Mdai LEO CORNEL AWITI h/b OLOF AWITI**

**Jina la Mdaiwa JORDAN STAUFFER WARIOBA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JORDAN STAUFFER WARIOBA**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**
**KUJIBU DAI LAKO LA TSHS. 7, 502,339/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 2 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 5:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KARIAKOO - ILAL
DAR ES SALAAM

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25184/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late STEPHEN MASAKA KULWA of Miyuji Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SABINA STEPHEN MASAKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

.................................................

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 11, 2024
Date at Dodoma this 5 Day of 11, 2024.

..................................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 5 day of 11, 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 26247 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE KENNETH OSWIN MILLINGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY RAHEL JOHN MAKELEMO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

.................................................

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 11, 2024
Date at Dodoma this 14TH Day of August, 2024.

..................................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 4 day of 11, 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA (W) – BOMANI**

**KUITWA SHAURINI**
**(MCA 84)**

**SHAURI LA MADAI NO.95/2024**

**MDAI ............................................KHALIFA B MBILINYI**

**DHIDI YA**

**MDAIWA...................................................SADICK SAID**

**Kwa SADICK SAID**

**Mdaiwa popote ulipo**

Shauri la madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama hii leo tarehe 11/11/2024 na shauri hili limepangwa kutajwa tarehe11/12/2024 saa 2:3 asubuhi. Hivyo basi unatakiwa wewe mdaiwa kuhudhulia hapa Mahakamani siku hiyo bila kukosa. Usipofika shauri litaendelea kusikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi ya upande mmoja.
Hati hii imetolewq kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26/11/2024.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

---


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## SWAPO yakabiliwa upinzani mkali uchaguzi wa Namibia

**WINDHOEK,** Namibia

IDADI kubwa ya raia wa Namibia ambao walishindwa kupiga kura kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ucheleweshaji wa vifaa waliendelea na zoezi hilo hadi usiku wa manane.

Maelfu ya Wanamibia walishiriki uchaguzi mkuu Jumatano, lakini ulikuwa na dosari nyingi za ucheleweshaji wa upigaji kura.

Kutokana na changamoto hizo, chama cha Upinzani IPC, kilitoa malalamiko kwa Tume ya Uchaguzi kikidai kuzuiwa wapiga kura kwa makusudi.

Licha ya baadhi ya wapiga kura kusubiri hadi saa 12 jioni kutokana na matatizo ya kiufundi, sheria za uchaguzi zilihakikisha bado wanaweza kuendelea kusimama kwenye foleni kwa ajili ya kupata nafasi ya kupiga kura zao.

Mgombea wa chama tawala cha SWAPO, Netumbo Nandi-Ndaitwah, ambaye anatarajia kupata ushindi mwembamba alihimiza watu kujitokeza kwa wingi.

Ndaitwah anakabiliwa na shinikizo kutoka kwa Wanamibia ambao wanalalamikia ukosefu wa ajira na usawa.

Wachambuzi wa kisiasa wanasema kuna dalili wagombea wa vyama hivyo viwili wakakosa ushindi wa jumla, hivyo kusababisha kuwepo kwa duru ya pili ya uchaguzi kwa mara ya kwanza tangu nchi hiyo ijipatie Uhuru. **DW**

## Rais Putin atishia kulipua majengo muhimu Ukraine

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, ametishia kuyashambulia majengo muhimu ya kutolea maamuzi yaliyoko katika mji mkuu wa Ukraine, baada ya msururu wa mashambulizi makali usiku wa kuamkia jana.

Akizungumza kwa mara ya kwanza akiwa katika mkutano wa kilele nchini Kazakhstan, Rais Putin, alisema majengo ya kufanyia maamuzi yanaweza kulengwa kwa kombora jipya la balestiki ambalo Russia ililitumia kushambulia mji wa Dnipro wa Ukraine wiki iliyopita.

Alisema nchi yake ilishambulia Ukraine kwa makombora 90 na ndege zisizo na rubani 100 usiku kucha wa jana kujibu mashambulizi ya kutumia silaha za Uingereza na Marekani wiki iliyopita.

„Tumefanya mashambulizi makubwa," alisema, na kuongeza kuwa vituo 17 vya kijeshi katika eneo la Ukraine vimepigwa.

Ali

Alisema Russia ilirusha makombora 100 na ndege zisizo na rubani 466 kwenda Ukraine katika siku mbili zilizopita.

Zaidi ya watu milioni moja nchini Ukraine hawana umeme baada ya kushambulia mitambo ya umeme ya nchi hiyo katika maeneo kadhaa. **BBC**

# Maelfu ya Walebanon warejea baada kuanza usitishwaji vita

**BEIRUT,** Lebanon

MAELFU ya raia wa Lebanon waliohamishwa makazi yao kutokana na vita kati ya Israel na Hezbollah, wamerejea nyumbani na kukaidi maonyo kutoka majeshi ya Lebanon na Israel kutogusa baadhi ya maeneo.

Kurejea kwa watu katika makazi yao yaliyoharibiwa na vikosi vya Israel, inafuatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali ya Israel na Lebanon kuhusu usitishaji vita hiyo iliyodumu kwa muda wa mwaka mmoja.

Vita hiyo kati ya wanamgambo wa Hezbollah na Israel vilisababisha kupanuka na kutishia kuingiza Iran katika mapigano.

Hata hivyo, mkataba huo hauzungumzii vita vya Ukanda wa Gaza, ambapo mashambulizi ya Israeli yalifanyika usiku wa manane kwenye shule mbili zilizokuwa makazi ya muda na kuua watu 11, wakiwemo watoto wanne.

Israel ilisema shambulio moja lililenga mlenga shabaha wa Hamas na lingine lililenga wapiganaji waliokuwa wanajificha miongoni mwa raia.

Mohammed Kaafarani, mwenye umri wa miaka 59, ambaye alihamishwa kutoka kijiji cha Lebanon cha Bidias alisema walikuwa na hali mbaya kiasi ambacho ilifikia hatua hakukuwa na mahali pa kujificha.

Mkataba ulioratibiwa na Marekani na Ufaransa, na kuidhinishwa na Israel jioni ya Jumanne, unahitaji kusitishwa kwa mapigano kwa muda wa miezi miwili na kuitaka Hezbollah kumaliza uwepo wake wa kijeshi katika eneo la kusini mwa Lebanon, pia wanajeshi wa Israeli wanapaswa kurudi upande wao wa mpaka.

Maelfu ya wanajeshi wa Lebanon na walinda amani wa Umoja wa Mataifa watapelekwa kusini, na jopo la kimataifa litakaloongozwa na Marekani litafuatilia utekelezaji.

Rais wa Marekani, Joe Biden, alisema utawala wake utatia msukumo mwingine wa kusitisha mapigano Gaza na kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas.

Hezbollah licha ya kupoteza sifa zake ilizozipata kwa kupambana na Israeli, bado iliweza kutoa upinzani mkali na kupunguza kasi ya vikosi vya Israeli kusonga mbele huku wakirusha roketi nyingi, makombora na ndege zisizo na rubani kuvuka mpaka kila siku. **AP**



Raia wa Palestina akiangalia jengo lililokuwa makazi yake likiwa limesambaratishwa na Israel katika mji wa Gaza jana. **PICHA: AP**

# Watu 30 wahofiwa kufariki dunia katika maporomoko ya udongo

**KAMPALA,** Uganda

WATU 30 wanahofiwa kufariki Dunia baada ya kutokea maporomoko ya ardhi katika kijiji kimoja mashariki mwa Uganda.

Hata hivyo, ofisa mmoja wa serikali alionya idadi hiyo huenda ikapanda kutokana na ukubwa wa tukio hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Bulambuli, Faheera Mpalanyi aliliambia shirika la habari la AFP, kuwa maporomoko ya ardhi yalitokea katika kijiji cha Masugu na kusababisha nyumba kufukiwa na vifusi vya udongo.

Mpalanyi alisema kutokana na uharibifu,ukubwa wa eneo lililoathirika na jinsi familia zilizoathirika zinalivyoeleza idadi kubwa ya watu hawajulikani waliko na kuna uwezekano wamefukiwa kwenye vifusi.

Msemaji wa Shirika la Msalaba Mwekundu la Uganda, John Cliff Wamala alisema miili 13 ilipatikana.

Alisema zaidi ya nyumba 40 zimeharibiwa kabisa na baadhi ya maeneo hayafikiki kutokana na mafuriko ya maji yaliyochanganyika na tope.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Uganda ilitoa tahadhari kupitia mtandao wa X, kuwa mvua kubwa iliyonyesha juzi Jumatano katika maeneo tofauti ya Uganda ilisababisha maafa katika maeneo mengi.

Taifa hilo la Afrika Mashariki limekumbwa na mvua kubwa katika siku za karibuni, huku kukishuhudiwa mafuriko katika eneo la kaskazini magharibi mwa nchi baada ya Mto Nile kuvunja kingo zake. **DW**

# CAMARA: MECHI ZA CAF SIO RAHISI

**Na Faustine Feliciane**

SHUJAA kwenye mchezo wa juzi wa Kombe la Shirikisho Afrika kwa upande wa Simba, golikipa Moussa Camara, amesema licha ya ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya klabu ya Bravos do Maquiz ya Angola, michezo ya CAF ni migumu hasa kwenye hatua ya makundi.

Juzi Simba ilifanikiwa kupata ushindi huo katika mchezo wa kwanza hatua ya makundi kwa bao pekee la mkwaju wa penalti lililofungwa na Jean Charles Aoua huku Camara akidaka mkwaju wa penalti.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Camara, alisema anashukuru kuisaidia timu yake kuibuka na ushindi lakini kazi haikuwa nyepesi.

"Haukuwa mchezo mwepesi, ni mchezo mgumu lakini ni furaha kuona tumepata ushindi, wapinzani wetu walibadilika sana kipindi cha pili lakini tulisimama imara," alisema Camara.

Aidha, alisema michezo hiyo kwenye hatua ya makundi si mepesi kwa kuwa kila timu inakuwa imejiandaa kikamilifu na zina ubora ndio maana zimefika hatua hiyo.

"Hakuna timu nyepesi kwenye hatua hii, kikubwa kwetu ni kujipanga kuhakikisha tunapata ushindi kwenye kila mchezo ili kuingia hatua inayofuata," alisema.

Mbali na kudaka penalti, Camara alikuwa kwenye kiwango cha juu kwenye mchezo huo ambapo aliokoa hatari nyingi golini kwake na kuihakikishia Simba kupata pointi tatu muhimu.




Nyota wa Yanga, Max Nzengeli akishuka kwenye ndege mkoani Mtwara akiwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo kitakachocheza na Namungo kesho kwenye uwanja wa Majaliwa. **PICHA: YANGA**

# Kocha Azam afurahishwa ushindani Ligi Kuu Bara

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema kwa muda mfupi aliofika Tanzania ameona ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu kitu anachokifurahia zaidi.

Akizungumza na Nipashe jana, Taoussi, alisema Ligi Kuu ni ngumu kutokana na kila timu kujiandaa na kuhitaji pointi tatu kitu kinachomfanya kuwa makini katika kuandaa timu yake kwenye kila mchezo.

"Nafurahia ushindani uliopo, kama kocha inakufanya kuwa macho muda wote kuelekea kwenye kila mchezo, unatakiwa kukiandaa vizuri kikosi kulingana na aina ya mchezo, Ligi ina ushindani sana," alisema Taoussi.

Alisema hata mchezo wao uliopita dhidi ya Kagera Sugar ili wabidi kupambana kwa dakika zote kuweza kupata ushindi.

"Tutaendelea kujiimarisha na kupambana kwenye kila mchezo ili kupata ushindi, nafurahishwa na namna wachezaji wangu wanavyojituma kuanzia mazoezini mpaka kwenye mechi," alisema.

Azam kwa sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 24 baada ya kucheza michezo 11 sawa na Simba wanaoongoza Ligi wakiwa na pointi 28.

Yanga yenyewe inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi sawa na Azam ikizidiwa magoli ya kufunga, hata hivyo mabingwa hao watetezi wana mchezo mmoja zaidi mkononi baada ya kucheza michezo 10.

## Kiungo Fountain Gate akiri kusimamishwa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya tetesi za wiki kadhaa kuwa baadhi ya wachezaji wa Fountain Gate wamesimamishwa kutokana na tuhuma za kucheza chini ya kiwango kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba Jiji Novemba 5, kiungo wa timu hiyo, Abalkassim Suleiman, amejitokeza na kukiri kusimamishwa.

Kiungo huyo amesema amesimamishwa kwa makosa mawili ambayo ni kutoroka kambini na kucheza vibaya kwenye mchezo dhidi ya Pamba Jiji waliofungwa mabao 3-1 huku yeye mwenyewe akilimwa kadi nyekundu.

"Habari hizo ni za kweli, nimepewa barua ya kusimamishwa kwa kosa la kuondoka kambini bila ruhusa lakini pia natuhumiwa kuwa nilicheza vibaya kwenye mchezo dhidi ya Pamba ambao nilionyeshwa kadi nyekundu, pia wanasema eti nilifanya makusudi kupewa kadi hiyo," alisema kiungo huyo.

Alisema baada ya siku kadhaa kupita aliwapigia simu viongozi kuomba kuonana nao kwa ajili ya kuzungumza ili kama ikiwezekana wavunjiane mkataba ili aondoke kwa amani na kusaka malisho mengine hasa kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

"Hivi karibuni niliwapigia simu viongozi juu ya sakata hilo niliomba kuonana nao ili wanipe barua ya kuachana na timu wamenitaka nikutane nao tena Desemba 6 mwaka huu kwa ajili ya kikao cha kunijadili," alisema.

Naye kocha wa makipa wa timu hiyo, Ally Mustapha ,Barthez', amekiri kusimamishwa lakini akiwa hajui sababu ni nini.

"Kwa sasa nipo Dar, nimeondolewa kwenye majukumu yangu sifahamu sababu ni nini, labda wao ndiyo wanajua," alisema Barthez ambaye aliwahi kuzidakia timu za Simba na Yanga kabla ya kugeukia ukocha.

Mwingine ambaye amesimamishwa ni golikipa, Fikirini Bakari, ambaye inasemekana aliruhusu kufungwa mabao rahisi katika mchezo huo na kuifanya Pamba Jiji kupata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu, tena ikiwa ugenini.



Hata hivyo, uongozi wa klabu hiyo umekuwa kimya na hautaki kuongea lolote kuhusu sakata hilo, wakati timu yao ikiwa inakamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 17.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARNOLD NA REAL MADRID
LIVERPOOL na Real Madrid zilifanya mazungumzo kuhusu mustakabali wa Alexander-Arnold kabla ya mechi ya wawili hao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano. (*Marca*)

### KERKEZ AZIVUTIA MAN, LIVER
MLINZI wa Bournemouth mwenye umri wa miaka 21 kutoka Hungary, Milos Kerkez anavutiwa na Manchester United na Liverpool. (***Sky Germany via Florian Plettenberg***)

### MAN UNITED YAWEKA ORODHA
KLABU ya Manchester United ina orodha fupi ya mabeki wengine watatu wa kushoto, akiwemo mchezaji wa kimataifa wa England na Chelsea mwenye umri wa miaka 27, Ben Chilwell, mchezaji wa kimataifa wa Algeria mwenye umri wa miaka 23, Rayan Ait-Nouri na Alvaro Carreras mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaichezea. Benfica. (***Rudy Galetti***)

### LIAM DELAP ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA inamtaka mshambuliaji wa Ipswich mwenye umri wa miaka 21, Liam Delap, lakini wanaweza kukabiliana na ushindani kutoka kwa klabu ya Manchester City. (***Football Insider***)

### DE JONG KUJIUNGA LIVERPOOL
KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 27, anaweza kujiunga na Liverpool msimu ujao wa majira ya joto. (***Fichajes***)

### BARCO KUSITISHIWA MKATABA
KLABU ya Sevilla inafikiria kusitisha mkataba wa mkopo wa beki wa Brighton mwenye umri wa miaka 20 kutoka Argentina, Valentin Barco Januari. (***Fabrizio Romano***)

### KILICSOY AIVUTIA VILLA, PSG
ASTON Villa bado inavutiwa na mshambuliaji wa Besiktas na Uturuki, Semih Kilicsoy, lakini italazimika kupambana na PSG kuwania saini ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 Januari. (***Star***)

### ADAM WHARTON BEI JUU
ARSENAL imefanya mazungumzo kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa England, Adam Wharton, huku Crystal Palace wakiweka bei ya euro milioni 65 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. (***Caught Offside***)

### MAN CITY WATAKA NYOTA
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amewataja kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 24 na winga wa Sporting wa Uruguay kama wachezaji anaolenga kuwasajili katika dirisha la uhamisho la Januari (***Fichajes***)

### ASTON VILLA YAVUTIWA NA AMIRI
KLABU ya Aston Villa inavutiwa na kiungo wa kati wa Mainz na Ujerumani, Nadiem Amiri mwenye umri wa miaka 28. (***Bild***)

### EDERSON AGOMBEWA EPL
KLABU za Manchester United, Manchester City na Liverpool zote zinamtaka kiungo wa kati wa Atalanta na Brazil, Ederson, lakini itahitaji ofa kubwa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (***TeamTalks***)

### KIWIOR KUONDOKA ARSENAL
FIORENTINA na Napoli zinatazamia mkataba wa mkopo kwa mlinzi wa Arsenal, Jakub Kiwior lakini kuna uwezekano kocha Mikel Arteta atamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 24 kuondoka Januari. (***Tuttomercato***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JOSHUA KIMMICH KUONGEZA MKATABA BAYERN MUNICH

## ●●●Mkataba wake wa sasa unamalizika majira ya joto na klabu za....

**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa kati wa Bayern Munich, Joshua Kimmich anakaribia kukubali kuongezewa mkataba mpya licha ya kutakiwa na Barcelona na Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa ripoti.

Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani unatarajiwa kumalizika msimu wa majira ya joto na kumekuwa na uvumi wa mara kwa mara juu ya mustakabali wake katika miaka ya hivi karibuni.

Kumekuwa na mazungumzo juu ya uhamisho wa bure kwa viongozi wa LaLiga Barcelona, huku miamba ya Ufaransa PSG pia ikihusishwa.

Kimmich mwenyewe hakuzima mazungumzo ya kuhamia Barca alipoulizwa Oktoba lakini maendeleo ya hivi karibuni yanaonesha kwamba anaweza kuishia kuongeza muda wake wa kukaa Allianz Arena.

**Gazeti la L'Equipe limeandika kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 sasa yuko karibu kuongeza mkataba wake na Bayern kuliko kuashiria nia yake ya kujiunga na PSG.**

Mazungumzo yanasemekana kuimarika zaidi ya wiki chache zilizopita na ripoti inaongeza „makubaliano yanakaribia kukamilika".

Kumekuwa na mabadiliko mengi chanya huko Bavaria katika miezi ya hivi karibuni.

Kuondoka kwa kocha Thomas Tuchel na kuteuliwa kwa Vincent Kompany kumeimarisha kikosi hicho, huku Kimmich akicheza mara kwa mara katika safu ya kiungo baada ya kutumia kiasi kikubwa cha kampeni zisizo na mafanikio za 2023/24 katika nafasi ya beki wa kulia.

Wakati Bayern wamerejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kupoteza mara mbili katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kunamaanisha kuwa wababe hao wa Ujerumani lazima wamalize hatua za awali kwa nguvu au wahatarishe kukosa nafasi ya nane bora, ambayo itawapa fursa ya kufuzu moja kwa moja kwa hatua ya 16 bora.

# ANCELOTTI: MBAPPÉ BADO HAJIAMINI



**LIVERPOOL,** England

CARLO Ancelotti amesema Kylian Mbappé anasumbuliwa na „kutojiamini“ baada ya fowadi huyo kukosa penalti wakati Real Madrid wakichezea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Liverpool kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi.

Mbappé alipata nafasi ya kusawazisha mchezo huo kuwa 1-1 katika dakika ya 61 baada ya Alexis Mac Allister kuiweka Liverpool mbele kwenye Uwanja wa Anfield, lakini mkwaju wake wa penalti uliokolewa na golikipa, Caoimhín Kelleher.

Mohamed Salah pia alikosa mkwaju wa penalti, kabla ya Cody Gakpo kufunga bao la pili la wenyeji kwa kichwa na kuifanya Liverpool kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Mabingwa na kuwaacha Madrid wakiwa katika nafasi ya 24.

“Inatokea sana kwa washambuliaji, kuna wakati ni ngumu kwao kufunga,“ alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

“Kuna tiba, na ni uvumilivu. Ni wakati mgumu kwake, zaidi ya yote leo (juzi), kwa kukosa penalti. Kila mtu anapaswa kumuunga mkono.

“Inaweza kuwa ukosefu wa kujiamini. Wakati mwingine unapokuwa na wakati ambapo mambo hayaendi sawa, wazo ni kucheza kwa urahisi, na unaweza kufanya mambo kuwa magumu kidogo. Amefunga penalti nyingi. Wakati mwingine unaweza kukosa moja.

“Lazima afanye kazi, aendelee kupigana, na nyakati hizi mbaya kwake zitapita.“

Mbappé sasa amefunga mabao mawili pekee katika mechi tisa zilizopita za Madrid katika michuano yote, na ameshindwa kufunga katika mechi nne zilizopita za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

“Anaonekana mzuri kwetu, anafanya mazoezi vizuri, anajiamini,“ alisema kiungo Luka Modric akiiambia Movistar.

“Wakati mwingine mambo hayafanyi kazi na wakati mwingine hayafanyiki. Leo (juzi) haikuwa hivyo, juu ya yote kwa penalti, lakini tunamwamini. Kylian atafanya kile kinachotarajiwa kutoka kwake, kwa hakika.“

# Amorim: Nitamsaidia Rashford

**MANCHESTER,** England

KOCHA mkuu wa Manchester United, Ruben Amorim amesema atamsaidia Marcus Rashford kurudisha kiwango chake bora, lakini akasisitiza kuwa mchezaji huyo pia anatakiwa kujituma kweli.

Rashford alifunga mara 30 katika mashindano yote msimu wa 2022/23, akiwa pia amefikia hatua ya mabao 20 katika msimu wa 2019/20 na 2020/21.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hajawa kwenye kiwango chake katika kipindi cha miezi 18 iliyopita.

Kumekuwa na matumaini kwamba nguvu mpya na mawazo mapya kufuatia kuteuliwa kwa Amorim yanaweza kuwa chachu, huku Rashford akifunga kwenye mchezo dhidi ya Ipswich Town Jumapili iliyopita.

Lakini United hawakuweza kuendeleza uongozi huo wa mapema na kuishia sare ya 1-1.


„Nitajaribu kumsaidia,“ alisema Amorim.

„Nafasi hiyo sio bora kwake, tunapaswa kuendelea na shinikizo la juu. Tutajaribu kutafuta suluhisho sahihi kwake, kama ilivyo kwa wachezaji wengine.

“Lakini inabidi Marcus kwanza kabisa yeye mwenyewe anatakiwa kujaribu kurejea kwenye kiwango chake. Kisha atapata msaada wa wafanyakazi wote, klabu na mashabiki kwa sababu yeye ni mtoto wa Manchester United lakini lazima ajitume.



# Slot afurahia kumaliza miaka 15 ya kufungwa



**LIVERPOOL,** England

KOCHA Arne Slot alisherehekea ushindi wa mabao 2-0 wa Liverpool wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid kwa kusema miamba hiyo ya Hispania imekuwa ikiwaletea maumivu na sasa wamemaliza kipindi cha miaka 15 bila ushindi dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ulaya.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Alexis Mac Allister na Cody Gakpo - huku Kylian Mbappé na Mohamed Salah wakikosa penalti, yalihitimisha ushindi kwa Liverpool na kuwafanya kuwa kileleni mwa msimamo.

Huku Liverpool ikishindwa kuifunga Madrid katika mechi sita zilizopita, zikiwemo fainali za Ligi ya Mabingwa mwaka 2018 na 2022, Slot alisema ni muhimu kuwafunga washindi hao mara 15 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

“Unajua jinsi ilivyo maalum kucheza dhidi ya timu ambayo imeshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nyingi,“ alisema Slot.

“Walikuwa wakituletea maumivu kwa miaka mingi. Ni wiki kubwa na inafurahisha.

“Nadhani ni vizuri kushinda mchezo na haswa mchezo mkubwa kama huu, unajua unakutana na wachezaji wengi wenye ubora.

“Lakini hii ni mpangilio wa kushangaza na tofauti katika Ligi ya Mabingwa na ni ngumu kuhukumu jinsi ushindi huu ni muhimu.

“Ikiwa tutakutana nao Madrid katika hatua ya 16 bora na kisha tukaweza kuwashinda itakuwa taarifa kubwa zaidi.“

„Sikuwa na ratiba kulingana na kiasi cha pointi nilichotaka,“ alisema.

“Unataka kutekeleza mtindo wa uchezaji haraka iwezekanavyo. Hilo sio gumu kwa sababu haikuwa tofauti na Jürgen Klopp (mtangulizi wake). Ni vyema kuona sio tu wanaoanza lakini pia wachezaji wanaokuja wanafanya kama tunavyotarajia.

Mechi inayofuata ya Liverpool itakuwa dhidi ya Manchester City kwenye Ligi Kuu England Jumapili.

## HABARI MICHEZO

### Yanga yapania kurejea kwa kasi Ligi Kuu Bara

INATOKA UKURASA 24

kuipambania timu yao," alisema Kamwe.

Alikiri kuwa ni kweli wanapitia kipindi kigumu, lakini bado hawana msimu mbaya kwani wamezidiwa pointi nne tu na wapinzani wao na kama wakipata ushindi na kufanana michezo, itasalia pointi moja tu.

Yanga inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu mpaka sasa ikiwa na pointi 24, sawa na Azam FC yenye pointi 24, lakini wanalambalamba wameruhusu mabao matatu, Wanajangwani wakiruhusu mabao manne.

### Fadlu alia na umaliziaji Simba

INATOKA UKURASA 24

wake nje.

Shujaa wa mchezo huo, golikipa Moussa Camara, aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kushangilia ushindi huo akisema haukuja kirahisi kwani wamepambana na kiasi kikubwa kuupata, badala ya kusikiliza watu wakilalamikia kiwango.

„Mechi ilikuwa ngumu, lakini tulikuwa nyumbani na tumeweza kupata ushindi, hiki ni kitu kizuri sana kwetu, kipindi cha kwanza tulikosa nafasi nyingi, kipindi cha pili wapinzani wetu walibadilika na mimi kama golikipa ilikuwa ni jukumu langu kuhakikisha naisaidia timu yangu," alisema Camara.

Akizungumzia mchezo ujao dhidi ya CS Constantine ya Algeria, alisema utakuwa mchezo mgumu, lakini watajipanga kwa ajili ya kwenda kusaka ushindi au sare.

„Tunaangalia sasa mchezo ujao, utakuwa mgumu kuliko huu, lakini tunakwenda kucheza kwa ajili ya kushinda mechi au sare, kikubwa ni kwenda kupambana," alisema Camara.

Simba itasafiri hadi Algeria kucheza mchezo wa raundi ya pili, Kundi A, hatua ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika kucheza dhidi ya CS Constantine Desemba 8 mwaka huu, Uwanja wa Mohamed Hamlaoui.



# HAPPINES MAGESE JAJI MKUU SAMIA FESTIVAL

**Na Faustine Feliciane**

MWANAMITINDO wa Kimataifa Happiness Magese jana ametangazwa kuwa Jaji Mkuu wa Tamasha la ubunifu la ‚Samia Fashion Festival' litakalofanyika kesho visiwani Zanzibar.

Akizungumza na waandishi jana baada ya kutangazwa kuwa Jaji Mkuu wa Tamasha hilo , Magese alisema kuwa ni heshima kubwa na furaha kwake kusimama kama Jaji Mkuu wa Samia wa Fashion Festival 2024 na anajivunia kushuhudia wakati huu wa kihistoria ambao unasherehekea ubunifu, stara, na urithi wa kipekee wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema yeye na wengine waliteuliwa kuwa majaji wanaamini tukio hilo ni kubwa na litakalobakia katika kumbukumbu zao kwa miaka mingi ijayo kutokana na kuteuliwa kwao kuwa majaji wa Samia Fashion Festival.

"Kwa zaidi ya miaka ishirini, nimejitolea maisha yangu katika sekta ya mitindo, urembo, nimezunguka duniani nikifanya kazi na chapa kubwa na maarufu, nimeona jinsi mitindo inavyothaminiwa katika nchi za Ulaya na mataifa mengine, si tu kama sanaa bali kama alama ya utambulisho, urithi, na fahari.

"Niliposikia kuhusu mpango huu wa kipekee, sikusita, nilichukua ndege haraka kuja nyumbani kuwa sehemu ya safari hii ya kihistoria kwa tamasha hili si tu kuhusu mavazi, ni kuhusu heshima yetu kama Watanzania,"alisema.

Mwanamitindo huyo ambaye anaishi nchini Marekani kwa sasa alisema uandaaji wa Vazi la Samia alama ya stara, uongozi, na heshima ni zaidi ya mavazi ya kawaida.

Ni kazi ya sanaa inayostahili kuhifadhiwa katika makumbusho kwa vizazi vijavyo, kama heshima kwa urithi wa kiongozi huyo.

Alieleza ilikuwa ni ndoto yake ya siku nyingi kuona Vazi la Samia linakuwa ishara ya kitaifa na kimataifa, chanzo cha fahari kinachowakilisha uzuri, nguvu, na umoja wa Tanzania.

"Tukubaliane kufanya kitu cha kipekee, kitu kitakachotupeleka ulimwenguni na kuacha alama katika historia. Kwa wabunifu, wanamitindo, na wote wanaoshiriki, tambueni kuwa hampo tu katika sehemu ya tamasha, bali mnakuwa sehemu ya historia ya kizazi kitakachovutia dunia. Hebu tufanye wakati huu uwe wa kukumbukwa milele", alisema Magese.

Mbali na Magese, wengine walioteuliwa kuwa majaji ni Idris Sultan ambaye ni Muigizaji na mchekeshaji mashuhuri, Khadija Mwanamboka ambaye ni mbunifu maarufu na mwanzilishi wa sanaa mbalimbali.

Wengine ni Jokate Mwegelo, Kiongozi mashuhuri na Malkia wa Urembo hapa nchini, Martin Kadinda ambaye ni Mbunifu maarufu wa mavazi, Faraja Nyalandu, Kiongozi wa Jami na Malkia wa Urembo pamoja Nancy Sumari.

Awali akizungumza kuhusu Samia Fashion Festival Mwanzilishi na Muandaaji wa Tamasha hilo, Mwanamboka alisema amewashirikisha wanamitindo mbalimbali na kuungana nao katika tamasha hilo ili Kusaidia watoto wanaoishi na virusi Vya UKIMWI na Saratani.



Mwanamitindo wa Kimataifa Happiness Magese (katikati) akizungumza na waaandishi wa habari jijini Dar es Salaaam baada ya kutangazwa kuwa Jaji Mkuu wa Tamasha la 'Samia Fashion Festival' ambalo limeandaliwa na Mwanamitindo Khadija Mwanamboka (kushoto), kulia ni Idris Sultan ambaye ni Mwigizaji maarufu nchini Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba SC, Yanga zawekwa kiporo FA

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limetoa ratiba kamili ya raundi ya tatu ya kombe la FA huku klabu za Simba na Yanga zikiwa hazijapangiwa tarehe za michezo yao kutokana na kuwa kwenye michezo ya kimataifa.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam, michezo ya raundi ya tatu inatarajiwa kupigwa kuanzia Desemba 5 mpaka 8 mwaka huu, lakini vigogo hao wakiwa wameondolewa kwenye ratiba kwani zote zitakuwa ugenini Algeria kucheza mechi za kimataifa.

Desemba 7, mwaka huu, Yanga itakuwa nchini Algeria kucheza dhidi ya MC Alger kwenye Uwanja wa Julliet wa Tano, saa 4:00 usiku kwenye mchezo wa Kundi A, Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Simba itacheza siku moja baadae (Desemba 8) saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui dhidi ya CS Constantine ya Algeria katika mchezo wa Kundi A, Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwenye mchezo wa raundi ya tatu ya FA, Yanga ilipaswa icheze dhidi ya Copco FC, huku Simba ikipangiwa dhidi ya Kilimanjaro Wonders Sports Center.

Kwa mujibu wa TFF, tarehe za michezo hiyo itapangwa baadaye huku timu zilizobaki zikitarajiwa kucheza kuanzia Desemba 5 hadi 8.

Azam FC inatarajia kukipiga dhidi ya Iringa Sports, Desemba 7 Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Singida Big Stars itakuwa Uwanja wa Liti, Singida kucheza dhidi ya Magnet FC, Mashujaa FC itawakaribisha mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1986, Tukuyu Stars kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, KMC itacheza na Black Six, Uwanja wao wa nyumbani, Fountain Gate itacheza dhidi ya Mweta Sports, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, Coastal Union itakuwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kuisubiri Stand United, Kagera Sugar na Rhino Rangers zitakipiga kwenye uwanja wa Kaitaba huku Dodoma Jiji ikikipiga na Leo Tena, Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Michezo ya raundi ya tatu itaendelea tena Desemba 8 ambapo Geita Gold itacheza na Ruvu Shooting, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, Prisons itacheza dhidi ya Tandika United Uwanja wa Sokoine, Mbeya wakati JKT Tanzania itaumana na Igunga United kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam.

# Michezo

**Nipashe** Ijumaa Novemba 29, 2024




**Kimmich kuongeza mkataba Bayern Munich** UKURASA 21

# Yanga yapania kurejea kwa kasi Ligi Kuu Bara

●●● Kocha Ramovic amesema tayari amerekebisha mapungufu na sasa....

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga jana mchana kiliwasili mkoani Lindi kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo unaotarajiwa kuchezwa kesho, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sead Ramovic, akiahidi kurejea kwa kasi ligi kuu baada ya kurekebisha mapungufu aliyoyaona kwenye mchezo uliopita wa Ligi ya Mabingwa Afrika, dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan uliochezwa Jumanne iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Yanga imewasili Lindi ikiwa na kikosi kamili tayari kuwafuta machozi mashabiki wake ambao wamekosa furaha baada ya kupata vichapo vitatu mfululizo katika mechi tatu zilizopita.**

Yanga walianza kufungwa kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC walipofungwa bao 1-0 na baadae kupata kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Tabora United kabla ya jumanne iliyopita kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal.

Akizungumza jana muda mfupi kabla ya kuanza safari ya kuifuata Namungo, Ramovic amesema kwa sasa wamefanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mchezo uliopita dhidi ya Al Hilal na sasa wapo tayari kwa mchezo huo wa kesho.

"Kama nilivyosema suala ya utimamu huwezi kulitatua kwa muda mfupi, lakini tumeanza kulifanyia kazi, na nadhani linaweza kukaa sawa baada ya muda, kwa sasa nataka turejee kwenye michezo ya Ligi kwa kasi" alisema Ramovic.

Mchezo huo wa leo, utakuwa wa kwanza kwa kocha huyo kuiongoza Yanga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu baada ya kuondoka kwa Miguel Gamondi ambaye aliipa ubingwa msimu uliopita na msimu huu aliiongoza kwenye michezo 10, ikishinda minane na kupoteza miwili.

Mara baada ya mechi dhidi ya Al Hilal, Ramovic alibainisha kuwa wachezaji wake walionekana hawana utimamu wa mwili pamoja na pumzi ya kucheza kwa dakika 90 kwa nguvu ile ile, hivyo kuahidi kulifanyia kazi suala hilo.

Katika hatua nyingine, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kusahau yaliyopita na kuganga yajayo akiwataka kujitokeza kwa wingi ili kuipa sapoti timu yao.

"Malengo yetu kwa sasa ni mchezo wa Jumamosi dhidi ya Namungo, ushindi ni muhimu sana kwenye mechi hii ili kupunguza pengo la pointi na anayeongoza. Tunajua muda ni mdogo sana ku-

INAENDELEA UKURASA 23



Ramovic

## Fadlu alia na umaliziaji Simba

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids amesema licha ya ushindi walioupata kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquiz, bado safu yake ya ushambuliaji imekuwa na tatizo la kukosa umakini kwenye umaliziaji.

Hata hivyo kocha huyo amesema wachezaji wake wanastahili pongezi kwa namna walivyopambana kwenye mchezo huo na kupata ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo wa juzi, Kocha huyo raia wa Afrika Kusini alisema anaenda kufanyia kazi mapungufu hayo ili mchezo ujao waweze kutumia nafasi wanazozitengeneza.

Alisema baada ya kukosa mabao mengi, wachezaji wake walionekana kucheza kwa wasiwasi ili wasikosee hivyo mechi ikaonekana ngumu.

"Nimefurahi kupata pointi tatu kwenye mchezo wetu wa kwanza, ila tungeongeza umakini kidogo tungetoka uwanjani na ushindi wa zaidi ya mabao mawili hasa kipindi cha kwanza, nawaamini wachezaji wangu wote kuanzia wa kwanza hadi wa 26, kila mmoja anaweza kucheza muda wowote, haya ni mashindano ambayo unatakiwa kuwa na wachezaji mbadala,"alisema Fadlu.

Alisema anaamini mchezo ujao watakuwa bora zaidi na kuwataka mashabiki kuendelea kuwaunga mkono wachezaji wao na kuwapa hamasa zaidi.

Pamoja na kupata ushindi wa bao 1-0, baadhi ya mashabiki na wachambuzi wameonekana kutoridhishwa na uwezo wa wachezaji wengi katika mchezo huo, huku pia wengine wakikosoa mabadiliko makubwa ya kikosi aliyoyafanya kwa kuwaacha baadhi ya nyota

INAENDELEA UK. 23

**Happines Magese jaji mkuu Samia Festival** UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >